epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Alhamisi Juni 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581706

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**TEN HAG SASA UHAKIKA KUBAKI MAN UNITED**



# Mchechu aja na undani kauli ya Rais Samia PSSSF

UKURASA 2

UKURASA WA 4

## KILICHOIBEBA NMB ONGEZEKO LA GAWIO

WANAHISA wa Benki ya NMB wameidhinisha gawio kubwa kuwahi kulipwa na taasisi hiyo la jumla ya Sh. bilioni 181 kutokana na...

UKURASA WA 17

## SMZ YACHUKUA HATUA KUKABILI UHABA WA DOLA

SERIKALI ya Zanzibar imechukua hatua za kukabiliana na uhaba wa dola zikijumuisha kuuza fedha za kigeni kwenye Soko la Jumla la...

UKURASA WA 4

## ACT KUIBURUZA TAMISEMI MAHAKAMANI

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kinakusudia kuishtaki Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali...

UKURASA WA 5

## SERIKALI YAPATA MBINU KUOKOA FEDHA UAGIZAJI MAFUTA NJE

KUTOKANA na matumizi makubwa ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza...



UKURASA WA 19


AJALI ZA NDEGE

## MIEZI 3 ZAACHA SIMANZI, WAMO RAIS NA MAKAMU

KWA miezi mitatu mfululizo ajali za anga zimetikisa dunia, huku zikisababisha vifo kwa..

# Macho na masikio kwa Dk. Mwigulu akitoa mwelekeo wa nchi

UKURASA 2



Wafungwa wakipiga kura katika moja ya nchi zinazoruhusu kundi hilo kupata haki hiyo. **PICHA: MTANDAO**




Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambengele

# Wafungwa, mahabusu gerezani kuandikishwa kuwa wapigakura

UKURASA 3

MICHEZO SINEMA YAKOLEA SIMBA SC UK.24 KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na mgombea urais wa Msumbiji kupitia Chama cha FRELIMO, Daniel Fransisco Chapo, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

MAPENDEKEZO BAJETI

# Macho, masikio makao makuu Dodoma

**Na Waandishi Wetu**

MACHO na masikio ya Watanzania leo yanaelekezwa Makao Makuu ya nchi Dodoma wakati Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25 yakisomwa, huku matarajio yakiwa ni kutoa kipaumbele kwenye mahitaji muhimu kama maji, umeme, elimu na miundombinu.

Machi 11, mwaka huu, serikali ilipendekeza ukomo wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2024/25 kuwa ni Sh. trilioni 49.34, sawa na ongezeko la asilimia 11.2 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/24 ya Sh. trilioni 44.3, huku asilimia 70.1 ikitarajiwa kutoka katika mapato ya ndani.

Akiwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya Bunge zima, Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba alisema kati ya mapato hayo, Sh. trilioni 29.9 yanatarajiwa kuwa ni makusanyo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema pia mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na wizara, taasisi na idara zinazojitegemea, yanatarajiwa kuwa ni Sh. trilioni 3.4 na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sh. trilioni 1,344.1.

"Sehemu kubwa ya bajeti asilimia 70.1 itagharamiwa na mapato ya ndani ambayo yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 10.0 mwaka 2024/25," alisema Nchemba.

**MIKOPO YA ELIMU**

Katika mwaka 2024/25, Mwigulu alisema kati ya Sh. trilioni 33.55 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 15.78 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, sawa na ongezeko la asilimia 3.8.

Pia, alisema fedha za maendeleo zinajumuisha ruzuku ya maendeleo ya Sh. trilioni 1.23 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya kati na ya juu pamoja na programu ya elimu msingi na sekondari bila ada.

Aidha, alisema utengaji wa fedha za maendeleo umezingatia miradi inayoendelea ikiwamo ya kimkakati na ya kielelezo pamoja na utekelezaji wa miradi kupitia utaratibu wa ushirikiano na sekta binafsi (PPP) ili kuipunguzia serikali mzigo wa kugharamia miradi ya maendeleo kwa utaratibu uliozoeleka.

Ili kufikia malengo na shabaha za utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25, Mwigulu alisema sera za mapato na hatua za kiutawala kwa mwaka 2024/25 zitalenga kuongeza makusanyo ya mapato kwa kuendelea, kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Ikiwa ni pamoja na kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa kero, kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari, kuongeza wigo wa kodi.

Pia, kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato, hususani kodi ya ardhi na pango.

Katika mwaka 2024/25, alisema serikali itaendelea kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria ya bajeti, sura 439, Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 ili kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kugharamia mahitaji yasiyoepukika ikijumuisha mishahara na deni la serikali.

Kadhalika, alisema serikali itaendelea kugharamia matumizi ya maendeleo yenye vyanzo mahsusi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo maalum yenye maslahi mapana kwa taifa kama vile Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Reli, Mfuko wa Umeme Vijijini na Mfuko wa Maji na Wakala wa Maji Vijijini.

Vile vile, alisema serikali itaendelea kuhakiki, kulipa na kuzuia ongezeko la malimbikizo ya madai pamoja na kufanya maboresho katika mfumo wa ununuzi wa umma ili kuhakikisha unakuwa wenye tija na kuendana na thamani ya fedha.

Mwanadiplomasia na mchambuzi wa siasa, Hamduni Maliseli, alisema kuwa bajeti ya mwaka huu itakuwa ya kihistoria kwa kuwa inaiingiza nchi katika uchumi wenye nguvu unaoonekana katika wingi wa fedha zinazoingizwa katika wizara mbalimbali ili kuunga mkono utendaji wa serikali.

Alisema bajeti hiyo inaakisi matarajio ya Watanzania kuwa inayotegemea mapato ya ndani kwa zaidi ya asilimia 70 na kwamba ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa fedha hizo zinafanya kazi kama zitakavyoelekezwa.

Alisema bajeti hiyo ikitekelezwa kama ilivyokusudiwa italeta mapinduzi katika sekta mbalimbali ikiwamo kilimo, elimu na uwekezaji hali itakayochangia kukuza kipato cha wananchi na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma, CPA David Mwakapala alisema bajeti hiyo imejikita katika kuimarisha miradi ya maendeleo hali inayoonyesha dhima ya serikali ya kumkomboa mwananchi katika kadhia mbalimbali.

Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, Visent Mbogo, alisema kuwa matarajio ya bajeti hiyo ni kuwagusa wananchi wa kipato cha chini wakiwamo wakulima wadogo, wafanyabiashara wa chakula na viwanda vidogo vinavyoajiri vijana.

Mbunge wa Viti Maalumu Tuza Malapo anasema ni matarajio yake kuwa yale mambo yote waliyoshauri kwenye mapato, matumizi, elimu, mifugo uvuvi na ukusanywaji wa kodi yatakwenda kufanyiwa kazi na kuleta unafuu wa maisha kwa wananchi.

Mkazi wa Korogwe vijijini, Janeth Msofe, alisema anatarajia bajeti hiyo kutoa kipaumbele Wizara ya Afya kwa kuwa inapitia changamoto nyingi hasa maeneo ya vijijini ambako bado kinamama wanatembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya ikiwamo kujifungua.

Mkazi wa Mwanza Mjini, Innocent Mtemi, alipendekeza bajeti hiyo itoe kipaumbele miradi endelevu kama vile treni ya umeme ya GSR na bandari kwa sababu vina mwingiliano wa moja kwa moja na shughuli za kiuchumi za wananchi.

***Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR) na Paul Mabeja, (DODOMA)**

# Mchechu aja na undani kauli ya Samia PSSSF

**Na Romana Mallya**

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu (pichani chini), amesema maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, hayakuwa katika kikokotoo ingawa yakifanyiwa kazi kwa kina na kuwa na matokeo chanya, yana nafasi ya kuleta ahueni katika jambo hilo.

Mchechu aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) baada ya hafla ya taasisi na mashirika ya umma kutoa gawio na michango kwa serikali.

Katika hafla hiyo iliyofanyika Ikulu, Dar es Salaam, Rais Samia alipokea gawio na michango kutoka kwa mashirika 145 yenye thamani ya Sh. bilioni 637.12, zikijumuisha gawio la Sh. bilioni 278.869 kutoka mashirika ya biashara na michango Sh. bilioni 358.254 kutoka taasisi zingine.

Rais Samia aliweka wazi kwamba kuna mashirika ambayo hesabu zake zinachechemea, lakini yana orodha ya miradi mingi yaliyoandaa kutekeleza, akiutaja Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) hauko vizuri.

Kutokana na hilo, Rais Samia alimweleza Msajili wa Hazina kwamba ana kazi na kumwagiza akasimamie mashirika ili wafanyakazi wakistaafu wapate fedha zao kwa wakati bila kusubiri kama walivyokubaliana kisheria.

Alipoulizwa wafanyakazi watarajie nini baada ya maagizo hayo ya Rais hasa suala la kikokotoo, Mchechu alisema maagizo ya Rais hayakuwa kwenye suala hilo.

"Lakini maagizo yake tukiyafanyia kazi kwa kina yakiwa na matokeo chanja yana nafasi ya kuleta ahueni katika kikokotoo ambacho ndio maslahi makubwa ya wafanyakazi waliowekeza akiba yao huko ili wakistaafu wapate maisha bora," alisema.

Mchechu alisema watu wanapokatwa fedha zao zinakwenda kwenye uzalishaji wenye tija ili kuwa na kiwango au ongezeko la mtaji kilichowekwa kuwasaidia wao na wengine wanaokuja kulipwa kilicho bora.

Alisema mapato mazuri yanatoka kwenye miradi mbalimbali au uwekezaji ambao taasisi hizo za pensheni zinakwenda kuwekeza kwenye miradi ambayo ipo katika uwekezaji wa hisa, hati miliki, dhamana za serikali ambazo zinaweza kuleta fedha.

"Ukiangalia uwekezaji uliofanywa na mifuko pensheni kulikuwa inayokwenda kwenye miliki ambapo kuna vitu au miradi mingine ambayo haikuwekwa vizuri, mapato si mazuri au inawezekana mipango ilikuwa mizuri wakati wa andiko la utekelezaji, lakini hawakusimamia vizuri, au mipango iliandikwa vizuri, lakini usimamizi na uadilifu haukuwa vizuri," alisema.

Kutokana na hayo, Mchechu alisema wanakwenda kufanya mambo mawili, kwanza kwa kutambua kuwa Rais ni taasisi hivyo wanakwenda kutekeleza maagizo aliyotoa.

Kadhalika, alisema kwa nafasi aliyo nayo ni moja wapo ya kazi ya msajili pale anapoona kuna changamoto au kuna kitu hakijakaa vizuri, sheria inamruhusu kuunda kamati, kuunda tume ya kuchunguza, kuomba nyaraka zozote na hata kuzuia matumizi fulani yanayofanyika.

Mchechu alisisitiza kwamba, katika maboresho wanayokwenda kufanya yatafanya ofisi hiyo kukalia vizuri kazi zake.



HABARI KITAIFA

# Wafungwa, mahabusu gerezani kuandikishwa kuwa wapigakura

Na Moshi Lusonzo

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imetangaza maboresho mapya ya uandikishaji wapigakura kwenye uchaguzi ujao, ikiwa na ubunifu wa njia za kidigiti.

Sambamba na hilo, mahabusu na wafungwa wenye kifungo chini ya miezi sita gerezani wataruhusiwa kuandikishwa kupiga kura.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Ramadhani Kailima (pichani), alifafanua hayo jana, akiutaja mfumo huo wa kidigiti unaoitwa 'Online Voters Registration System (OVRS)', unalenga kurahisisha maboresho ya taarifa za wapigakura.

Kailimu alikuwa anawasilisha mada kuhusu maandalizi ya uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura awamu ya kwanza kwa wahariri na waandishi wa habari jana Dar es Salaam.

Aliitaja kuwa ni kanuni ya 15 (2) (c) ya Kanuni za Uboreshaji Daftari la Kudumu la Wapigakura za Mwaka 2024, inayowezesha wafungwa au wanafunzi waliohukumiwa kifungo cha chini ya miezi sita na mahabusu gerezani kuandikishwa kuwa wapigakura.

Pia alisema kwa Tanzania Bara kuna vituo vya kuandikisha wapigakura 130 vilivyoko kwenye magereza na kwa Zanzibar kuna vituo 10 kwenye vyuo vya mafunzo.

Kuhusu Diaspora kupiga kura, alisema sheria bado haijatungwa na kwamba ikifika wakati imetungwa, basi wataruhusiwa kushiriki mchakato wa uchaguzi na kwamba matumizi ya vitambulisho vingine yatafanyika kadiri mifumo ya kisheria itakavyoona kama kuna urahisi wa kuvitumia.



Hata hivyo, wapigakura ambao wanaandikishwa mara ya kwanza watapaswa kwenda kwenye vituo 40,126 vilivyoko Tanzania Bara na Zanzibar.

Kailima alisema mpigakura aliyeko kwenye daftari, anaweza kuanzisha mchakato wa kubadilisha taarifa ama kuhama jimbo, kata au kubadilisha na kuhama kituo cha kupigia kura kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta.

Alisema mfumo wa uandikishaji wapigakura umefanyiwa usanifu na kuboreshwa ili kukidhi aina ya BVR Kits za sasa ambazo zinatumia programu endeshi ya Android ambayo ni tofauti na iliyotumika awali kupitia programu za Windows.

"Mpigakura anayerekebisha taarifa zake kwa njia ya mfumo huu ni sharti awe na namba ya NIDA," alibainisha.

Pia alisema kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, wapigakura wapya 5,586,433 wanatarajiwa kuandikishwa ambao ni sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 walioko kwenye daftari baada ya uboreshaji uliofanyika mwaka 2019/2020.

Alisema wapigakura 594,494 wataondolewa kwenye daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwapo, huku baada ya maboresho hayo inatarajiwa daftari litakuwa na wapigakura 34,746,638.

Kwa mujibu wa Kailima, idadi inaweza kuongezeka kwa kuwa inawezekana wako Watanzania ambao walikuwa na sifa za kuandikishwa kuwa wapigakura wakati wa maboresho lakini kwa sababu mbalimbali hawakujiandikisha.

"Tume imekamilisha idadi ya vituo vya kuandikishia wapigakura jumla yake ni 40,126. Kati ya hivyo, 39,709 viko Tanzania Bara na 417 viko Zanzibar. Hilo ni ongezeko la vituo 2,312 kulinganisha na vituo 37,814 vilivyokamilika 2019/20," alisema.

Uboreshaji wa majaribio ulifanyika katika Kata ya Ng'ambo, Manispaa ya Tabora na Kata ya Ikoma Halmashauri ya Wilaya ya Rorya mkoani Mara, alisema lengo lilikuwa kujaribu utayari na ufanisi wa vifaa vipya vitakavyotumika wakati wa uboreshaji wa daftari.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa maboresho hayo, tume iliandaa mifumo na taratibu mbalimbali kama maandalizi ya kuanza uboreshaji unaotarajiwa kuanza Julai mosi mwaka huu.

Awali, akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa INEC, Jaji Jacobs Mwambegele, alisema uboreshaji wa daftari la wapigakura hautafaulu kwa kiwango walichojipangia kama wanahabari hawatachukua jukumu lao la msingi la kuelimisha umma kujitokeza vituoni.

Aliwapongeza wahariri na vyombo vya habari kwa kufanya kazi kubwa ya kuwaunganisha tume na wananchi na kusababisha chaguzi zote zilizofanyika kwa kutumia mfumo huo wa upigaji kura kuwa na ufanisi.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Wakazi wa Mtaa wa Mdote, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakiwa wamepanga foleni ya kuchota maji jana kwa sababu ya kutoka mara moja kwa wiki. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kilichoibeba NMB kuongeza gawio wanahisa kwa asilimia 26

**Na Mwandishi Wetu**

WANAHISA wa Benki ya NMB wameidhinisha gawio kubwa kuwahi kulipwa na taasisi hiyo la jumla ya Sh. bilioni 181 kutokana na faida baada ya kodi ya mwaka ulioisha Desemba 31, 2023.

Hilo ni ongezeko la asilimia 26 kulinganishwa na gawio la Sh. bilioni 143 la mwaka 2022. Gawio la bilioni 181 ni sawa na gawio la Sh. 361 kwa kila hisa.

Ongezeko hilo la mwaka mzima la kampuni linaashiria mapato mazuri na endelevu kwa wanahisa, uongozi wa benki hiyo ukitangaza kuwa gawio litalipwa Juni 19 mwaka huu au siku chache kabla na baada ya tarehe hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki hiyo, wamepata faida kabla ya kodi ya Sh. bilioni 770 na faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 542, zote zikiwa ni ongezeko la asilimia 26 mwaka hadi mwaka.

"Ufanisi huu kiutendaji ni matokeo ya nidhamu ya utekelezaji mkakati wa benki, ukuaji thabiti wa mapato, udhibiti wa gharama na kuimarika kwa ubora wa mikopo.

"Viwango hivi vya faida ni vipya na vikubwa katika historia ya benki na tasnia ya huduma za kifedha nchini, vinavyoimarisha dhamira ya benki ya kuwapa thamani stahiki wadau wake," ilisema taarifa ya benki hiyo iliyotolewa kwa vyombo vya habari.

Mwaka 2023, jumla ya mapato ya benki yalikuwa zaidi cha Sh. trilioni 1.4, sawa na ongezeko la asilimia 18 kutoka Sh. trilioni 1.2 za mwaka 2022. Ukuaji huo matokeo ya kuimarika ukuaji mapato yatokanayo na riba (NII), yaliyoongezeka kwa asilimia 19 hadi Sh. bilioni 934 kutoka Sh. bilioni 786 zilizopatikana mwaka 2022 kutokana na kuongezeka mikopo na uwekezaji katika dhamana na serikali.

Benki pia ilipata ukuaji mzuri wa mapato mengine (NFI) yaliyoongezeka kutoka Sh. bilioni 402 mwaka 2022 hadi kufikia Sh. bilioni 468, ikiwa ni ukuaji wa asilimia 16 mwaka hadi mwaka kutokana na wateja kutumia zaidi mifumo ya huduma za kidijitali.

Vilevile, benki ilikuwa na mafanikio makubwa kiufanisi na kuimarisha utoaji mikopo. Uwiano wa gharama na mapato (CIR) uliimarika hadi kiwango bora cha asilimia 39 huku uwiano wa mikopo chechefu ukibaki kuwa asilimia 3.2.

Takwimu hizo zilikuwa chini ya ukomo wa juu wa kikanuni wa asilimia 55 na asilimia tano, mtawalia. Benki imeendelea na kuboresha mizania yake kwa ajili ya kuongeza mapato yanayotokana na mali inazomiliki.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mizania iliimarika zaidi kwa jumla ya mali kufikia rekodi ya Sh. trilioni 12.2, sawa na ukuaji wa asilimia 19 kulinganishwa na Sh. trilioni 10.2 mwaka 2022.

Ukuaji imara wa mizania unatokana na ukuaji mkubwa wa asilimia 28 ya mikopo kwa wateja, uwekezaji makini katika dhamana za serikali uliokua kwa asilimia 17, pamoja na kukua kwa asilimia 11 mwaka hadi mwaka kwa amana za wateja.

Akizungumzia malipo hayo ya gawio, Mwenyekiti wa Bodi ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alisema:

"Uimara wa misingi ya uongozi na utawala bora, dhamira yetu katika kutengeneza thamani endelevu kwa wadau wote pamoja na msisitizo mkubwa katika ajenda ya uendelevu, ni baadhi ya nyenzo muhimu zinazoendelea kuchochea ukuaji endelevu wa Benki ya NMB kwa sasa na miaka mingi ijayo.

"Kwa mwaka wa fedha 2023, wanahisa wameidhinisha gawio la fedha taslimu Sh. 361 kwa kila hisa, sawa na gawio la jumla la Sh. bilioni 181, ambayo ni sawa na theluthi moja ya faida halisi kulingana na Sera ya Gawio ya Benki ya NMB.

"Gawio linalopendekezwa kwa kila hisa limeongezeka kwa asilimia 26 kutoka Sh. 286 kwa hisa lililolipwa mwaka uliotangulia (2022). Matarajio yetu ni kuzidi kuimarika kwa dhamira yetu ya kutoa mapato bora ya kifedha na yasiyo ya kifedha kwa wadau wetu.

"Bodi itaendelea kutoa usimamizi stahiki na kuichagiza Menejimenti ili NMB iendelee kutengeneza thamani."

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema utekelezaji Mpango Mkakati wa Muda wa Kati wa Miaka Mitano (MTP) unaendelea vizuri kama inavyothibitishwa na maendeleo thabiti ya mipango ya kimkakati.

"Ili kuendelea kuaminiwa sokoni na kuiongezea kasi ajenda ya ujumuishaji kifedha, tumepanua mtandao wetu kwa kufungua matawi mapya manne na kuongeza zaidi ya mawakala wapya 11,000, hivyo kufikia mawakala 28,295 mwaka 2023.

"Kutokana na hilo, tuliweza kusajili akaunti mpya za wateja zaidi ya milioni 1.2. Juhudi zetu za kuunda benki ya uhakika ya siku zijazo, inayoendeshwa kiteknolojia na uwekezaji mkubwa tunaofanya kwa watu wetu unaendelea kutoa matokeo chanya," alisema.

Zaipuna aliongeza: "Mafanikio ya mwaka huu yanadhihirisha mchango na jukumu endelevu la NMB katika ustawi wa kiuchumi na kufungua fursa mpya kwa wateja na wadau wote.

"Kwa hakika tunajivunia imani ya wateja na wanahisa wetu pamoja na kujitoa kwa wafanyakazi wetu, ambao wametusaidia kufikia hatua hizi muhimu za kihistoria.

"Tunaendelea kuzingatia utekelezaji ajenda yetu ya uendelevu na kujitolea kugusa maisha ya watu na kuwezesha jamii. Mwaka 2023, tuliwekeza zaidi ya Sh. bilioni 6.2 katika mipango yetu ya urejeshaji kwa jamii na uendelevu, kwa kujikita zaidi katika elimu, afya, ujasiriamali pamoja na mazingira na masuala ya tabianchi."

Zaipuna alisema kuwa mwaka huu wametenga Sh. bilioni 5.4 kutoka kwenye faida yao ya mwaka 2023 baada ya kodi ili kuendelea kusaidia jamii.

Alitoa shukrani kwa bodi, wanahisa, wasimamizi wa sekta benki, serikali, wateja na wafanyakazi kwa kuendelea kuiamini na kuiunga mkono benki hiyo.

"Benki itaendelea kuzingatia utekelezaji mpango mkakati wake, ubunifu, ushirikishaji jamii na kuwapa wateja suluhisho bora za kifedha kwa ustawi wa pamoja," alisema Zaipuna.

## Madeni watumishi wa umma yafikia bil. 285/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema hadi kufikia Aprili 30, mwaka huu, madeni ya watumishi wa umma yaliyohakikiwa na kukidhi vigezo vya kulipwa yanayohusu likizo, uhamisho na kusafirisha mizigo baada ya kustaafu yalikuwa Sh. bilioni 285.1

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwan Kikwete, alisema hayo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Kibamba (CCM), Jumanne Mtemvu.

Katika swali hilo, Mtemvu alitaka kujua hadi sasa serikali ina madeni kiasi gani ya watumishi wa umma yanayohusu likizo, uhamisho, na kusafirisha mizigo baada ya kustaafu.

Kikwete alisema hadi Aprili 30, madeni ya watumishi wa umma yaliyohakikiwa na kukidhi vigezo vya kulipwa kwa ajili ya mambo hayo yalikuwa Sh. bilioni 285.1

Kadhalika, alisema katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, mwaka huu, madeni ya Sh. bilioni 55.9 yalikuwa yamelipwa.

"Aidha, serikali itaendelea kulipa madeni ya watumishi yasiyo ya kimshahara kila mwaka kwa kuzingatia taarifa ya uhakiki wa madeni," alisema Kikwete

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum, Ritha Kabati (CCM), alitaka kujua ni kwa kipindi gani mtumishi wa umma anatakiwa kudai madeni yake ya kusafirisha mizigo, likizo na uhamisho.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene alisema tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani ametoa Sh.bilioni 167.9 kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi wa umma .

Alisema madeni mengi yanazalishwa na mamlaka ya serikali za mitaa ambapo amewaomba Wabunge kushughulikia madeni hayo.

"Serikali ya Awamu ya Sita imejitahidi sana kulipa madeni ambapo hadi sasa tumelipa zaidi ya sh.bilioni 167.9 lakini bado mzigo unazidi kuongezeka kwasababu kule wanakozalisha madeni bado kuna uzembe,"alisema.

## HABARI KITAIFA

# PM aagiza taasisi kuhamia nishati safi ya kupikia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza taasisi zote za umma, kuacha matumizi ya kuni na mkaa na kuhamia kwenye nishati safi ya gesi, umeme na makaa ya mawe.

Aidha, amewaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji na Majiji, kuepuka migongano na migogoro yenye maslahi binafsi katika utangazaji na utoaji wa zabuni.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana jijini hapa, wakati akifungua mkutano mkuu wa 14 wa Taasisi ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania (TOA).

"Rais Dk. Samia Hassan amekuwa kinara wa uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia katika ukanda wa Afrika, hivyo taasisi zote za umma zikiwamo magereza, shule za bweni na vikundi vya kupika vyakula kwenye sherehe mbalimbali muanze kuachana na matumizi ya nishati ya kuni kwani inaharibu mazingira yetu," alisema.

Kwa mujibu wa Majaliwa, tamanio la serikali ni kufikia asilimia 80 ya Watanzania wote kutumia nishati safi ifikapo mwaka 2034.

Kuhusu migongano ya maslahi binafsi inayosababishwa na baadhi ya watumishi wa umma nchini hasa kwenye utangazaji na utoaji wa zabuni, alisema suala hilo halikubaliki.

"Maslahi binafsi hayakubaliki wakurugenzi wa halmashauri hakikisheni mnasimamia maslahi ya umma katika maeneo yenu ili wananchi wapate huduma bora kwa wakati," alisema.

### UCHAGUZI

Aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kusimamia maboresho ya daftari la kupiga kura pamoja na kuhamasisha watu wote waliofika umri wa kupiga kura kujiandikisha ili wapate haki yao ya kikatiba ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani.

"Nendeni mkahamasishe kikamilifu maboresho ya daftari la kupiga kura ili wananchi wenye sifa ya kupiga kura wapate haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi watakaowaletea maendeleo," alisema.

### RUSHWA

Majaliwa aliagiza Sekretarieti ya TOA kuhakikisha ajenda ya rushwa inajadiliwa kwa nguvu zote na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) watoe mada bila kuwaonea haya, wala kuwafumbia macho washiriki.

"TAKUKURU toeni mada ya rushwa katika mkutano huu muhimu kwa sababu ajenda hii ni muhimu na ijadiliwe kwa kina bila kuwaonea haya wala kuwafumbia macho washiriki," alisema.

# Serikali yapata mbinu kuokoa fedha uagizaji mafuta nje

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na matumizi makubwa ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta kwa ajili ya magari nje ya nchi, serikali imeanza mikakati kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo.

Moja ya mikakati hiyo ni kuhamasisha matumizi ya magari yanayotumia gesi asilia, kutoa msamaha wa kodi kwenye mitungi ya kuhifadhi gesi iliyoshindiliwa kwenye magari na kupunguza ushuru wa magari yanayotumia gesi asilia.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima, aliyetaka kujua ni lini serikali itakuja na mkakati wa kutumia gesi asilia kuendesha magari ili kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta nje ya nchi.

Akijibu swali hilo, Kapinga alisema serikali ilishaanza programu mbalimbali za matumizi ya gesi iliyogandamizwa (CNGO kwenye magari.

Alisema mpaka sasa serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imefungua vituo vitano na inatarajia kufungua vituo vingine vitatu ifikapo Desemba, 2024.

"Aidha, jumla ya vituo 16 (vituo mama viwili na vituo vidogo 14, vikijumuisha vituo vinavyohamishika vinatarajiwa kufunguliwa ifikapo Desemba, 2025." Alisema.

Alisema ili kuongeza upatikanaji wa gesi asilia, mwaka 2022 Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) ilifunga seti tatu za kompresa zilizoongeza mgandamizi wa futi za ujazo milioni 20 na kwa sasa TPDC imeanza utaratibu wa kumpata mzabuni kwa ajili ya kufunga mitambo ya kuongeza mgandamizo wa gesi yenye futi za ujazo milioni 20 kwenye kitalu cha uzalishaji cha Songosongo na kazi inatarajia kukamilika Machi, 2026.

"Tunaamini mikakati yote hii itachangia kuongeza idadi ya magari yanayotumia gesi nchini itakayosababisha kupunguza uagizaji wa mafuta nje ya nchi na mwisho kuokoa fedha za kigeni," alisema Kapinga.

Katika swali lake la nyongeza, Gwajima alihoji ni lini wakati mwafaka ambao serikali itafungua vituo vya gesi asilia ambavyo vitakuwa na wamiliki wa magari pembezoni mwa barabara.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kapinga alisema mkakati wa serikali ni kuanza kujenga vituo vya kujaza mafuta pembezoni mwa barabara ya Dar es Saalam hadi Dodoma kwa awamu ya kwanza.


**MATOLEO MAALUM**



The Guardian NA Nipashe

**KWA USALAMA WA TANZANIA IJAYO**

Miaka 5 ya Benkibima (Bancassurance), Ujenzi wa Sekta Inayoshamiri na Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima Nchini

Sekta ya bima nchini inakua kwa kasi kubwa. Katika kuelezea mafanikio hayo Kampuni ya The Guardian Limited (TGL), itachapisha matoleo maalum katika magazeti yake ya **The Guardian** na **Nipashe** mwezi ujao yatakayojikita kuangalia upatikanaji huduma za bima zenye matokeo chanya kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Matoleo hayo yatajikita zaidi kuelezea:

- **Mafanikio ya Benkibima kwa Kipindi cha Miaka Mitano**
- **Jitihada za Kitaifa Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima**
- **Mwelekeo wa Sekta ya Bima katika Serikali ya Awamu ya Sita**

Mradi huu wa ujumuishi wa huduma za kifedha ni jukwaa linalotoa fursa ya kipekee kwa watoa huduma za bima na wadau wengine kuonesha jinsi wanavyochangia ongezeko la upatikanaji huduma za bima na mapokeo yake nchini.

Usikose kutumia nafasi hii adimu kunadi taasisi yako na suluhisho bunifu dhidi ya majanga.

**Ili kupata maelezo zaidi ya jinsi ya kushiriki:**
**Wasiliana nasi kwa simu: 0714 791747, 0763214317, 0753 01427**
**Barua Pepe: advertise@guardian.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msako wa TBS viwanda uende zaidi ya malengo

**SHIRIKA** la Viwango Tanzania (TBS), limetangaza kuanza msako kwa wazalishaji wa chuma ili kuwachukulia hatua wale wanaotengeneza bidhaa zisizokidhi viwango kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Athuman Ngenya, alibainisha hayo mapema wiki hii wakati wa mkutano kati ya shirika hilo na wadau katika ofisi za shirika hilo, Ubungo, Dar es Salaam. Alisema miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa dhidi ya wamiliki wa viwanda hivyo ni kuvifungia iwapo vitabainika kutengeneza bidhaa zisizokidhi viwango kama sheria inavyotaka.

Katika taarifa yake hiyo, mkurugenzi mkuu huyo alibainisha kuwa moja ya matakwa muhimu ya viwango vya bidhaa za chuma zinazozalishwa au kuingizwa nchini ni pamoja na kuandikwa taarifa zinazoonyesha jina la mzalishaji na ukubwa wa bidhaa. Alisema taarifa hizo ni muhimu kwa wanunuzi na watumiaji wa bidhaa kwa kuwa huwezesha kutoa mrejesho kwa mzalishaji husika na kufanya ufuatiliaji endapo itabainika kuna kasoro yoyote.

Pia alibainisha kwamba uwapo wa taarifa muhimu kwenye bidhaa huziwezesha taasisi za udhibiti kuwa na uwezo wa kuzitambua, kuzifanyia ufuatiliaji katika soko na kuchukua hatua stahiki kwa mzalishaji atakayebainika kukiuka matakwa ya sheria, kanuni na viwango.

Pamoja na matakwa hayo ya kisheria na kanuni, alibainisha kuwa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa watumiaji wa bidhaa kwamba baadhi zina kasoro, hivyo kulifanya shirika hilo kufanya ufuatiliaji kuanzia maeneo zinakozalishwa. Kuwapo kwa tatizo hilo, alisema wazalishaji hao wamesababisha changamoto katika udhibiti na hasara kwa watumiaji, hivyo TBS haitasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya yeyote atakayezalisha bidhaa kinyume na matakwa ya viwango.

Hatua ya TBS ambayo kwa hakika hufanywa mara kwa mara na kubaini matatizo katika bidhaa mbalimbali, imetangazwa wakati mwafaka kwa kuwa hivi sasa kuna viwanda vingi vinavyotengeneza bidhaa za chuma. Kuna wasiwasi mkubwa kama watengenezaji wa bidhaa hizo wanafuata matakwa ya kisheria kupitia TBS kuhusu viwango na ubora unaotakiwa.

Nia ya TBS ni nzuri katika kuhakikisha Watanzania wanatumia bidhaa zenye viwango vilivyothitishwa na taasisi hiyo ya serikali ili kumlinda mtumiaji wa mwisho ambaye ni Mtanzania wa kawaida.

Kwa mantiki hiyo, TBS inapaswa kupewa ushirikiano kutoka taasisi za kiserikali ambazo zimepewa dhamana ya kusimamia sheria kama vile Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kubaini kama wazalishaji hao wanalipa kodi zinazotakiwa katika shughuli kama hizo.


Pamoja na kwamba chuma ni moja ya bidhaa zinazolalamikiwa na wananchi kuhusu ubora na viwango, kuna bidhaa zingine ambazo zina madhara makubwa kwa wananchi kama vile vyakula na vinywaji kama havitadhibitiwa ipasavyo.

Matumizi ya vinywaji kama pombe kali ambazo zimebainika kuwa nyingi hazina ubora zimekuwa zikitengenezwa na watu binafsi na viwanda bubu katika maeneo mbalimbali. Matokeo ya kuwapo kwa bidhaa hizo ambazo zinatengenezwa kinyemela ni kuwasababishia madhara makubwa watumiaji hasa wale wanaoshindwa kubaini bidhaa halali na isiyo halali.

Kwa mantiki hiyo, ukaguzi wa bidhaa uliopangwa kufanywa na TBS unapaswa kujikita katika bidhaa zote badala ya chuma pekee ili kuwalinda watumiaji ambao ni wananchi. Ni dhahiri kwamba kwa kufanya msako wa bidhaa zote, TBS kwa kushirikiana na polisi, TRA na mamlaka za serikali za mitaa, kutaibua mambo mengi na kuwachukulia wote wanaotengeneza bidhaa zisizokidhi viwango na kuweka rehani maisha ya Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanasiasa acheni 'bla blaa', hamasisheni kuandikisha wapigakura uchaguzi ujao

Na Mwandishi Wetu

**WAKATI** Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) imetangaza kuanza kwa uboreshaji wa daftari la wapiga kura nchini mwezi ujao, kumekuwa na mikutano ya wanasiasa katika maeneo mbalimbali nchini, ili kutetea ulaji wao katika mitaa.

Pilikapilika za wananasiasa hao zimeshika kasi, wakati ikiwa zimesalia miezi kadhaa wananchi kupiga kura kwa ajili ya kuchagua viongozi wa serikali za mitaa nchini kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

Mikutano hiyo imeanza kushika kasi katika siku za hivi karibuni, kwa baadhi ya wanasiasa wakiwemo wawakilishi wa wananchi kwenye mitaa, kata na majimbo nchini kuitishia mikutano ya wao kwa wao, kwa ajili ya kuwekana sawa, ili kujihakikishia ushindi.

Katika mikutano hiyo ya wawakilishi wa wananchi, wamekuwa wakihimizana na kupanga mikakati ya kuhakikisha wanaendelea kutetea nafasi zao na kujihakikishia ushindi kwenye nafasi za uenyekiti.

Hapo wanaelekezana jinsi ya kuwaelimisha wananchi utekelezaji wa miradi ya maendeleo na miundombinu katika maeneo yao, kama njia ya kuwashawishi kuendelea kuwachagua katika uchaguzi huo utakaofanyika baadaye mwaka huu kwa kuvishirikisha vyama vingi vya siasa.

Katika kuwekana sawa, wawakilishi hao wanakosoa tabia ya baadhi yao, kuunga mkono watu wanaowakashifu wenzao vijiweni ambako kuna makundi ya watu wanaolalamika huduma duni kwa kuwataja moja kwa moja viongozi kutokana na huduma duni.

Badala yake, wanaelekeza jinsi ya kupangua hoja zenye mijadala mibaya dhidi ya viongozi, wanasiasa kwa kuvutia upande wao kwa kusifia mazuri yanayofanyika katika jamii.

Wakati hayo yakijiri, wawakilishi hao wa wananchi wanasahau kuwa jamii inalalamikia huduma duni katika maeneo yao na kutaka kupatiwa ufumbuzi.

Jamii hiyo imekuwa ikilalamika kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara kutokana na kuharibika vibaya na hadi nyingine kugeuka mahandaki.

Ubovu huo wa Barabara, umesababisha maeneo mengi kukosa usafiri kutokana na magari kushindwa kupita huku nyingine zikigeuka madimbwi kutokana na kujaa maji yanayotokana na mabomba kupasuka.

Pamoja na kero hizo sugu kuliko zote, ni kuzagaa kwa takaa kwenye makazi ya watu, kutokana na magari kushindwa kwenda kwenye maeneo hayo, hasa mijini, kusomba na kupelekwa kutupwa kwenye madampo.

Vilevile kuna kuwapo mlundikano wa takataka kwenye makazi, kunahatarisha kutokea kwa mlipuko wa magonjwa yanayoenezwa na nzi na wadudu wengine. Magonjwa hayo yanaweza pia kuwakumba watoto wadogo wanaocheza kwenye maeneo ziliko takataka na kusambaa kwa kasi kwa watu wengine.

Chakushangaza, wawakilishi hao husani wajumbe ambao wanaishi kwenye maeneo hayo na wananchi, lakini wanashindwa kuchukua hatua zozote za kukabiliana na changamoto hizo badala yake wanaibuka msimu unapokaribia uchaguzi.

Hapo wanaanza kupita huku na kule wakihaha kushawishi wananchi kuchagua vyama vyao vya siasa ili kuwaongoza katika kipindi kingine.

Sisi wanajamii sasa tunahoji wawakilishi wetu, kama hawaguswi na kero hizo, tunawashangaa kwa kuendelea kutulaghai kwa kusaka ulaji kwa kuendesha mikutano hiyo katika maeneo yao. Badala yake, wawakilishi wangetumia muda wao huo kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika uboreshaji wa daftari hilo badala ya kujipanga kupangua hoja na malamiko dhidi yao kwa manufaa ya jamii.

Kuhamasisha wananchi kujiandikisha kupiga kura ni jambo muhimu zao kwa sababu ndio wakati wake ili kupata idadi kubwa ya wananchi watakaojitokeza kuchagua viongozi wao katika kipindi kijacho.

Baada ya kufanikisha hilo la kuhamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari hilo ambalo limekuwa likifanyika unapokaribia uchaguzi huo na ule mkuu, ndipo ufuate utaratibu mwingine ikiwemo wanasiasa kuelekezea utekelezaji wa miradi ya maendeleo, huduma za afya na mambo mengine mengi.

Wananchi ni mashahidi wa yale yanaendelea katika maeneo yao, hata wanafunzi wa shule za msingi wanasikika wakicheka na kuwabeza wawakilishi hao kwa kutoa ahadi kibao, ikiwa ni pamoja na kuweka taa barabara za mitaani na kuhoji wameshindwa kutengeneza barabara, huku maji yakitiririka ovyo babarabani watawezaje kufanikisha hilo.

Kwa mtindo huo msije mkashangaa mkizomewa kwenye mikutano yenu, mnapopita barabarani na hata mnapojinadi na wagombea wenu. Jamani jirekebisheni, ndugu zetu wanasiasa.

HABARI KITAIFA

# Raia wa China ahukumiwa jela miaka mitatu

Na Grace Gurisha

RAIA wa China, Zheng Zhiyua (47), amehukumiwa kulipa faini ya Sh. 300,000 au kifungo cha miaka mitatu gerezani.

Hukumu hiyo dhidi yake ilitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya, baada ya kukiri mashtaka matatu ya kuishi nchini bila kibali na kumtishia kwa kisu ofisa wa Idara ya Uhamiaji wakati akiwa kazini.

Wakili wa Serikali kutoka Uhamiaji, Grace Nyarata, alidai kuwa mshtakiwa huyo anatuhumiwa kuishi nchini bila kibali na alikutwa akifanya biashara bila kibali na pia alimtishia kwa kisu ofisa uhamiaji.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Lyamuya alisema mahakama imemtia hatiani Zhiyua kwa mashtaka yote matatu baada ya kukiri kutenda makosa hayo kama alivyosomewa na upande wa mashtaka.

Kutokana na kukiri mashtaka, alisema kila shtaka atatakiwa kulipa faini ya sh 100,000 na akishindwa kulipa fedha hizo atatumikia kifungo cha miezi 12 kwa kila kosa na akishatekeleza mojawapo ya hayo mawili arudi nchini kwao.

Awali, Nyarata alidai kuwa Juni 4, 2024 mshtakiwa akiwa eneo la Keko, Temeke mkoani Dar es Salaam, raia huyo wa China alikutwa anaishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila hati halali au nyaraka yoyote ya kuhalalisha uwapo wake.

Ilidaiwa katika siku na eneo hilo, Zhiyuan alikutwa akimzuia Ofisa Uhamiaji kutekeleza majukumu yake kwa kumtishia kisu na kukataa kuonyesha hati yake ya kusafiria huku akijua kitendo hicho ni kinyume cha sheria.

Alidai kuwa katika shtaka la tatu, siku na eneo hilo, mshtakiwa alikutwa akijihusisha na biashara katika duka lake bila kibali halali cha kuishi nchini ambacho kingempatia pia ruhusa ya kufanya biashara.

Baada ya mshtakiwa huyo kusomewa mashtaka dhidi yake, alikiri kutenda makosa hayo ndipo Hakimu Lyamuya alimsomea adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, mshtakiwa alikwenda mahabusu huku akiendelea kusubiri kukamilisha utaratibu wa kulipa faini.

**Mahakama imemtia hatiani Zhiyua kwa mashtaka yote matatu baada ya kukiri kutenda makosa hayo kama alivyosomewa na upande wa mashtaka.**



Watuhumiwa kesi ya kuvunja na kuiba, Elizabeth Ghati (wa pili kulia) na wenzake wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, kabla ya kusomewa mashtaka Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Watu wenye ualbino wamwangukia Samia

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHAMA cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS) kimeomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati ukatili unaoendelea dhidi ya jamii hiyo ili kuwa na amani.

Mwenyekiti wa Taifa wa TAS, Godson Mollel, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika ufunguzi wa watu wenye ualbino yanayofanyika Mailimoja, Kibaha mkoani Pwani.

Mollel alisema kwa muda mrefu sasa watu wenye Ualbino baadhi wanaouawa na wengine kujeruhiwa na hata kesi zikienda mahakamani hakuna anayekutwa na hatia jambo ambalo linasababisha kuendelea kwa vitendo vya kikatili dhidi yao.

"Tunamwomba Rais akutane na sisi tutafute mwarobaini wa tatizo hili. Tunachoomba kama mauaji yaliyokuwa yanatokea Kibiti yalivyodhibitiwa, ya watu wenye ualbino yataisha na sisi tutaishi kwa amani," alisema.

Pia alisema chama hicho kinamwomba Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, kupitia Bunge analoliongoza, kulaani ukatili unaoendelea dhidi ya kundi hilo kwa kuwa nao ni sehemu ya wapigakura wao. Pia aliomba viongozi wa dini wakemee suala hilo kwenye nyumba za ibada.

Alisema maadhimisho hayo ambayo yanafanyika duniani kote kila mwaka na hapa nchini yanaendelea kutumika kama sehemu ya kutoa elimu kwa jamii kutambua kwamba watu wenye ualbino hawana tofauti na wengine.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkuu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Joy Maongezi, alisema serikali inaendelea kusimamia sera, sheria na miongozo kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata haki zao.

Maongezi alisema bado jamii haina uelewa kuhusiana na watu wenye ualbino jambo ambalo linaifanya serikali kuendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye maadhimisho kama hayo.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Shangwe Twamala, akifungua maadhimisho hayo, alisema huduma mbalimbali za watu wenye ualbino zitatolewa, hivyo wazazi wenye ndugu na watoto wa kundi hilo, wajitokeze kuwapeleka kwenye eneo hilo.

Naye mratibu wa afya wa watu wenye ualbino kutoka Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Mohamed Chanzi, alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, kwa kuridhia maadhimisho hayo kufanyika katika mkoa wake.

Alisema tatizo kubwa kwa watu wenye ualbino ni afya na elimu inatolewa kwa wazazi na walezi kujua namna ya kijikinga na jua ambalo linawasababishia madhara kwenye ngozi zao.

Watu wenye ualbino kutoka mikoa mbalimbali nchini, wamefika Kibaha kushiriki maadhimisho hayo huku wengi wao wakisema wanashindwa kuishi kwa ndugu zao kwa kuhofia kuwaingiza kwenye matatizo endapo watatokea watu wa kuwafanyia ukatili.

Hivi karibuni, ziliripotiwa taarifa za kujeruhiwa kwa watu wenye ualbino katika mikoa ya Geita na Kagera na kwa mujibu wa viongozi, tangu mwaka 2000, kesi za ukatili na mauaji ya wenye ualbino zilizofikishwa mahakamani lakini hakuna aliyewahi kuhukumiwa.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# WMA yafanya msako kushtukiza lumbesa

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Vipimo (WMA), imefanya ukaguzi wa kushtukiza katika masoko mbalimbali jijini Dar es salaam ili kubaini mwitikio wa wafanyabiashara katika ufungashaji sahihi wa mazao kwa mujibu wa sheria ya vipimo.

Meneja wa Mkoa wa Kivipimo wa Ilala, Mhono Nashon, alisema wakala imefanya operesheni hiyo ikiwa ni mwendelezo wa mapambano dhidi ya ufungashaji holela wa mazao (lumbesa) ambao ni kinyume na sheria na kanuni za vipimo.

Alisema sheria na kanuni za vipimo zinamtaka mkulima au mfanyabiashara kufungasha mazao katika uzito usiozidi kilogramu 100 kwa mzigo mmoja.

Alisema katika ukaguzi huo, WMA imetembelea masoko ya Mabibo, Ilala na Stereo (Temeke) na kubaini mwitikio chanya wa wafanyabiashara na mazao ya viazi, vitunguu, karoti na mboga katika masoko hayo yamefungashwa kwa mujibu wa sheria ya vipimo katika uzito wa kilogramu 100.

Aidha, alisema WMA imeendelea kuwafikia wadau na wafanyabiashara katika maeneo yao na kuwapa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo ili kuleta usawa kati ya mtoa huduma na mteja na kuwalinda dhidi ya madhara yatokanayo na matumizi yasiyo sahihi ya vipimo.

Alisema WMA Mkoa wa Ilala imeandaa utaratibu wa kuwafikia wadau na wafanyabiashara katika soko la Ilala na kuwapa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo kwa ustawi chanya wa biashara.

Aliwaambia viongozi wa soko la Ilala kuwa mpango huo wa utoaji elimu utakuwa endelevu na kumfikia kila mdau na mfanyabiashara katika maeneo yake ya utoaji huduma.

" Ili kuhakikisha matumizi sahihi ya vipimo katika maeneo mbalimbali ya biashara ni lazima tutoe elimu ya matumizi sahihi ya vipimo na sheria zake, tutakuwa na siku 14 maalum za kutoa elimu kwa kila mdau na mfanyabiashara, tutapita kila kitalu, ghala na maeneo ya biashara na kutoa elimu hii," alisema

Aidha, alisema baada ya hapo yeyote atakaye kiuka sheria na kanuni za matumizi sahihi ya vipimo atakutana na mkono wa sheria ambapo kutakuwa na adhabu ya faini au kupelekwa mahakamani.

"Kwa hiyo viongozi wa soko fikisheni ujumbe huu kwa wafanyabiashara, nendeni mkawe mabalozi wazuri wa matumizi sahihi ya vipimo," alisema Nashon

Naye Meneja wa WMA Mkoa wa Kinondoni, Lilian Mwombeki, alitoa adhabu ya faini kwa wafanyabiashara wanne kwa kosa la kukiuka sheria ya vipimo na ufungashaji sahihi wa mazao kwa kufungasha mzigo wenye uzito wa zaidi ya kilogramu 100.

Adhabu hiyo ilitolewa kutokana na kaguzi za kushtukiza zilizofanya na WMA Mkoa wa Kinondoni katika soko la Mabibo ambapo watuhumiwa hao wanne walibainika kufungasha mzigo kiholela (lumbesa) katika nyakati tofauti huku wakifahamu kuwa ufungashaji huo ni kinyume cha sheria.

"Tunaendeleza mapambano dhidi ya lumbesa, naona asilimia kubwa ya wafanyabiashara sokoni hapa wametii sheria na wanafunga mizigo yao katika uzito usiozidi kilogramu 100, nawapongeza kwa hatua hii lakini kuna hawa wafanyabiashara wanne leo ninawapa adhabu ya faini kutokana na kosa la ufungashaji wa lumbesa ili iwe funzo kwa wengine wenye nia ya kufanya kosa kama hilo," alisema

"Naomba tushirikiane kutokomeza lumbesa kwa manufaa yetu wenyewe na jamii kwa ujumla," alisema Lilian akiwaambia wafanyabiashara katika soko la Mabibo.



Ofisa Vipimo wa Wakala wa Vipimo (WMA), Felix Juma (kushoto), akifanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye Soko la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana, kwa kupima magunia ya viazi kama yamefungashwa uzito usiozidi kilogramu 100 kwa mujibu wa sheria ya vipimo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Maofisa ugani wasisitizwa kutoa suluhu

**Na Maulid Mmbaga**

MAOFISA ugani wamesisitizwa kutoa majawabu ya changamoto zinazowakabili wakulima, wakiwamo wanaojihusisha na kilimo cha nazi na kuwafanya waone umuhimu wa kuwako kwa wataalamu hao katika kufanya kilimo endelevu na chenye tija.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Khadija Ally, wakati wa programu maalumu iliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Mikocheni, ikilenga kushirikishana elimu na ufahamu wa kitaalamu kuhusu kilimo cha nazi chenye tija.

Ally alitoa rai hiyo baada ya wakulima wa nazi katika wilaya hiyo kudai kwamba uhaba wa watalaamu wanaoweza kutoa mbinu za kisasa za kilimo hicho ni sababu ya zao hilo kukosa hamasa hususani kwa vijana.

Pia walisema hata maofisa ugani wachache walioko katika maeneo yao, wanatumia muda mwingi kushinda ofisini badala ya kuwatembelea wakulima mashambani kuwapa elimu ili kuwasaidia kutatua changamoto zinazowakabili.

Mkuu huyo wa wilaya alisisitiza wataalamu hao kuwa na ubunifu katika kufanya kazi hiyo kuwa rahisi lakini pia na faida na kwamba wasisubiri mkulima awafuate katika ofisi zao. Aliwataka kuwa na utaratibu wa kuwatembelea kila baada ya muda ili kusikiliza na kutoa majawabu ya kitaalamu kuhusu changamoto zinazohusiana na kilimo.

"Lazima maofisa ugani pamoja na wakulima mkutane nusu ya safari. Wananchi waone umuhimu wa msaada wako katika jambo uliloletwa kulifanya, lakini ukisema mimi watanifuata hapana. Inawezekana wakachelewa kukupata au wasijue kwamba kuna mtaalamu yuko kijijini.

"Weka utaratibu wa kukaa vikao na wakulima wako angalau kila baada ya miezi miwili. Mkutane mzungumzie fursa ambazo zipo, mikakati ya serikali na kupanga mambo yenu binafsi. Kwa utaratibu huo, mambo yatakwenda vizuri. Lazima tuwe na namna ya kufanya kazi hizi ziwe rahisi lakini pia ziwe na matunda. Zingatieni hilo ili kuleta tija," alisisitiza.

Meneja wa TARI Mikocheni, Dk. Fred Tairo, alisema kituo kimekuwa na programu ya kuwasaidia wakulima katika masuala mbalimbali ya kitaalamu pamoja na kuongeza tija, huku akiwashauri kuachana na utaratibu wa kuuziana nazi shambani badala yake wawe na utaratibu maalum ili kuongeza thamani.

"Nasisitiza katika suala la kuongeza thamani ya bidhaa hii kwa sababu nazi ile ya kula nyumbani ambayo ataiuza kwa Sh. 800 hadi 1,000, hiyo hiyo ndiyo inayotumika kutengeneza mafuta ambayo sokoni gharama yake itamnufaisha zaidi mkulima na kituoni kwetu tumeboresha mashine za kukamua na kuchuja mafuta.

"Mkulima baada ya kuvuna nazi zake anaweza kuja kuchukua mashine ile ambayo ataitumia kuchuja mafuta na hatimaye kuyahifadhi katika vifungashio maalumu na kwenda kuuza kwa bei nzuri itakayomfanya apate faida zaidi kwa sababu uhitaji wa bidhaa hiyo sokoni ni mkubwa tofauti na uzalishaji wake," alishauri Tairo.

Gideon Mwendiumi, mkulima anayemiliki ekari 11 za nazi wilayani Mkuranga, alitoa rai kwa serikali kuongeza nguvu kuwekeza zaidi katika teknolojia ya kilimo itakayosaidia kurahisisha shughuli hizo na kuvutia vijana wengi kujihusisha.

# Bajaji umeme kupunguza vifo vya nishati chafu

**Na Halfani Chusi**

MABADILIKO kutoka bajaji za kutumia mafuta kwenda za umeme yametajwa kuwa yatapunguza madhara yanayo sababishwa na nishati chafu ikiwamo vifo.

Hayo yalisemwa jana mkoani Dar es Salaam na Mchumi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Julius Ndele, wakati wa uzinduzi wa bajaji hizo zinazotengenezwa na kampuni ya TRI nchini.

Mei 27, mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo. katika mkutano na waandishi wa habari alisema zaidi ya watu 32,000 kila mwaka nchini hupoteza maisha kutokana na matumizi ya nishati chafu.

Ndele alisema bajaji hizo zitasaidia kupunguza athari za kimazingira zitokanazo na nishati chafu pamoja na kupunguza gharama za usafiri kwa wahitaji.

"Manufaa amabayo nchi itapata kutokana na teknolojia mpya ya bajaji za umeme ni mengi, kwanza zitasaidia kuongeza ajira kwa vijana, kuchochea ukuaji wa uchumi, lakini pia kuliweka jiji safi," alisema Ndele.

Aidha, aliwataka madereva wa bajaji kuchangamkia fursa hiyo huku akisisitiza kuwa zina tofauti katika gharama za uendeshaji na zile zinazotumia mafuta na gesi.



# TARI yagundua mbegu mpya za maharage

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TAASISI ya Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Seliani, imegundua aina mbili mpya za mbegu za maharage zenye viinilishe vya madini chuma na zinki, kuimarisha afya kwa wananchi na kukinzana na magonjwa yanayoshambulia mimea.

Hayo yalisemwa juzi na Mtafiti Mwandamizi wa Kilimo, Dk. Papias Binagwa kwenye Siku ya Mkulima iliyoandaliwa na taasisi hiyo iliyofanyika Kijiji cha Apakitete, Wilaya ya Karatu mkoani Arusha.

Dk. Binagwa, alisema utafiti na ugunduzi wa mbegu hizo ni matokeo ya utekelezaji wa Programu ya Mifumo Himilivu ya Chakula (TFSRP).

Mradi huo wa majaribio unatekelezwa na TARI kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB).

Alisema katika utekelezaji wa programu hiyo, TARI Seliani ina jukumu la kutafiti ugunduzi na uvumbuzi wa mbegu bora za kilimo zinazostahimili ukame, magonjwa, mavuno mengi na kukomaa kwa haraka.

Alisema majaribio ya maharage hayo ambayo yako kwenye hatua za mwisho kuingizwa sokoni, yamefanyika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Wilaya ya Karatu.

Alisema kwa Karatu, wamepeleka aina tatu za mbegu maharage, mbili kati ya hizo ziko hatua ya mwisho ya kuidhinishwa Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI) na nyingine sokoni.

"Lengo ni kuhakikisha teknolojia hii inawafikia wakulima wa Wilaya ya Karatu waweze kutumia mbegu bora kuongeza tija katika uzalishaji wa maharage," alisema Dk. Binagwa.

Alizitaja mbegu zinazotarajiwa kuingizwa sokoni baada ya kuidhinishwa na TOSCI kuwa ni RWR 2154 yenye madini ya chuma na zinki na kustahili ukame na NUA 64 inayostahimili magojwa na kuwa na wingi wa mazao.

Siku hiyo ya mkulima iliambatana na wakulima kupatiwa mafunzo ya kilimo bora na cha kisasa.

Katika mafunzo hayo, Ofisa Kilimo Wilaya ya Karatu, Wayda Sulle, alisema elimu ya matumizi ya mbegu bora, viuatilifu na upimaji wa udongo vitawasaidia wakulima kuongeza uzalishaji, kukuza kipato na kuwa na uhakika wa chakula kwa kaya.

"Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la watu na maeneo ni yaleyale, kuzalisha kwa wingi na kupata chakula cha kutosha watu wengi, tunashauri wakulima watumie mbegu bora zilizoletwa na watafiti," alisema Sulle.

Baadhi ya wakulima wa Kijiji cha Apakima Matete, John Silaa na Selina Barhe, walisema sifa za maharage hayo zinawapatia matumaini mapya kwa sababu zitaendana na hali ya hewa ya eneo lao lenye baridi.

Mdhibiti Mkuu wa Ubora wa Elimu wa Wilaya hiyo, Samson Mkonyi, alisema matokeo hayo ya tafiti zilizofanywa na TARI Selian ni hatua ya msingi kukamilisha ndoto za Rais Samia Suluhu Hassan za kuifanya Tanzania kuwa ghala la chakula.

## Shirika lataka kampeni familia kujumuishwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeshauriwa kuanzisha kampeni maalum ya kuhamasisha kujumuishwa katika ngazi ya uamuzi kuanzia kwenye familia hadi serikalini.

Ushauri huo ulitolewa mjini hapa juzi na Mkurugenzi wa Shirika la Voice Of Empowed Women (VOE-WOF), Asifiwe Mallya wakati akizungumza na makundi maalum katika Kata ya Boman'gombe Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro.

Mallya, alisema wananchi wanatakiwa kuelewa hakuna ujumuishwaji wa mwanamke peke yake na kuwataka kuondoa dhana hiyo ili kufikia maendeleo.

Mallya, alisema bado jamii ina ukakasi katika ujumuishaji, hivyo kundi moja kuendelea kukosa uwakilishi sahihi.

"Ujumuishaji unasaidia kuondoa unyanyapaa, ujinga, kutengwa hasa kwa jamii ya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo ni muhimu kwa wizara kuja na mkakati maalum wa kutoa elimu kuhusiana na ajenda hii," alisema. na kuongeza kuwa:"

Uwekezaji ni mchakato na ili ufanikiwe ni lazima mwanamke ajumuishwe na ahusishwe katika mchakato mzima. Maendeleo endelevu yanakuwa na maana pale ambapo hakuna watu au kundi la watu linaachwa nyuma. Tunajadili mambo muhimu ambayo yatakuwa na mchango muhimu katika dira ya taifa ya mwaka 2050."

Mkurugenzi wa Shirika la Ability & Disability in Tanzania, William Kivuyo, alisema lengo lao ni kuonyesha kila mtoto mwenye ulemavu anapata huduma zote za afya kuimarisha mahusiano.

"Tunafanya hivyo kwa kuwawezesha na kuungana na wawezeshaji wengine katika shule na kanisa, hospitali na jamii kwa ajili ya kuweka wigo mpana wa kuwasaidia wenye ulemavu au watoto wenye ulemavu ambao wanakosa huduma hizo za kuboresha maisha yao," alisema Kivuyo na kufafanua kuwa:



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kwamkabara, wilayani Muheza, Mkoa wa Tanga, Juma Hango (kulia), akikagua ujenzi wa choo cha matundu nane kwa ajili ya wanafunzi shuleni hapo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Maabara kukuza TEHAMA PAPU

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi, amezindua maabara ya kisasa kwa ajili ya kulisaidia Shirika la Umoja wa Posta Afrika (PAPU) kukuza Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utoaji wa huduma.

Mahundi, alizindua maabara hiyo ya kisasa yenye kompyuta 30 jijini Arusha juzi baada ya kufungua Mkutano wa 42 wa Baraza la Utawala la PAPU linaloundwa na nchi 45 wanachama wa umoja huo.

Mkutano huo uliuhudhuriwa na wadau wa sekta ya Posta Barani Afrika na wajumbe wa Sekretarieti ya Umoja wa Posta Duniani.

"Maabara hii itakuwa na tija kwa PAPU, likiwemo shirika letu la Posta nchini kutengeneza mifumo itakayoboresha mifumo ya Posta Afrika kuwa ya kidijitali na kufanya biashara za kimataifa ya kusafirisha vifurushi na vipeto kwa muda mfupi," alisema

Kuhusu Baraza la Utawala la PAPU, alisema katika mkutano wao huo wa siku mbili watajadiliana namna bora ya kuboresha uendeshaji wa Posta Afrika.

"Matumaini yangu kuwa kila nchi mwanachama wa PAPU tutaendelea kutumia mfumo wa kidijitali zaidi huduma zetu ambao utasaidia kufanya biashara mtandao katika ukanda wa nchi za Afrika na nje," alisema

Awali Katibu Mkuu wa PAPU, Sifundo Moyo, alisema mkutano huo pia watapokea taarifa ya kamati nne za wataalamu ili kuweka mipango yenye manufaa kwa umoja huo.

"Kamati hizo ni za fedha na utawala, uendeshaji na teknolojia, mikakati na ya sera na kanuni. Tunaimani maoni na mapendekezo watakayoyawasilisha yatasaidia PAPU kusonga mbele zaidi hasa katika masuala ya teknolojia," alisema

Posta Masta Mkuu, Maharage Chande, alisema uendeshaji wa huduma za posta kidijitali, utasaidia wananchi wa hali ya chini kufanya biashara kwa njia ya mtandao kwa kutumia shirika hilo kusafirisha vifurushi vyao ndani na nje ya nchi.

"Shirika la Posta Afrika tumeanza kutengeneza duka mtandao ili kukuza huduma zetu kimataifa, lakini maabara iliyozinduliwa itawezesha wananchi wa hali ya chini kufanya biashara zao mtandao na watasafirisha biashara hizo kupitia shirika letu la Posta kupitia mfumo wetu wa kidijitali na biashara ya aina hii imeshika kasi kwa sasa," alisema Chande.





# Shule na mdau wabadilishana miti 29 kwa madawati hamsini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SHULE ya Msingi Mhongolo iliyopo Kata ya Mhongolo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imebadilishana na mdau wa maendeleo miti 29 iliyokuwa imepandwa shuleni hapo kwa madawati 50.

Akipokea madawati hayo, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Ernest Peter, mbele ya Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mhongolo, Emmanuel Nangali, alisema madawati hayo ni matokeo ya miti iliyopandwa kwa ajili ya kulinda mazingira ya shule, sasa imekomaa na kuwapatia madawati 50 ambayo yanakwenda kutumiwa na wanafunzi.

Shule hiyo ina wanafunzi 2,500 na walimu 35 ambao pia hawakidhi mahitaji kulingana na wingi wa wanafunzi hao, kati ya idadi hiyo wanafunzi 70 ndiyo wanaokaa chini hususani wa darasa la tatu na nne.

"Miti hii ilipandwa miaka mingi kuzunguka mazingira ya shule na wanafunzi ndio walikuwa wanaihudumia mpaka kufikia sasa inakatwa na kuleta faida ya madawatu 50, alipatikana mtu akihitaji miti hiyo, hivyo tukaingia naye ubia wa kubadilisha kwa madawati ambayo yanakwenda kuondoa adha ya wanafunzi 70 kukaa chini," alisema Peter.

Alisema shule hiyo pia inakabiliwa na uhaba wa matundu ya vyoo, kutokana na idadi ya wanafunzi waliopo haiendani na miundombinu.

Alisema hivyo waliamua kukaa kikao na wazazi, kamati ya shule na serikali ya mtaa, ambao muafaka waliyokubaliana ni kuchangishana Sh.3,000 kila mmoja na sasa wameanza kuchimba shimo la choo, hivyo aliwaomba wadau wengine wa maendeleo kujitoa na siyo kuiachia serikali kila kitu.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mhongolo, Emmanuel Nangali, alisema upandaji wa miti unafaida kubwa licha ya kupata hewa safi, kivuli na matunda na sasa shule imeweza kupata madawati 50 pamoja na meza mbili.

Alisema kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini wameweza kupanda miti zaidi ya 300 kuzunguka eneo la shule hiyo, hadi sasa ipo katika hatua nzuri za ukuaji jambo ambalo linaleta matumaini ya miti hiyo kuwaletea manufaa ya kuuza au kutengeneza viti, meza na madawati ya shule.

Hivyo, aliwataka walimu kuendelea kuisimamia na kuhakikisha miti haishambuliwi na wanyama.

Mkazi wa mtaa huo, Clement Masonga, aliipongeza bodi ya shule kwa kuchukua hatua ya kubadilishana miti 29 na kupata madawati ambayo yatasababisha watoto wao kutoendelea kukaa chini wakati wa masomo, hivyo inaonyesha watafanya vizuri katika masomo maana watakuwa wamepata sehemu nzuri ya kukaa.



Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Shinyanga, wakiwa kwenye semina ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga juzi. Mradi huo hadi sasa umefikia asilimia 29 ya utekelezaji wake. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vibaka wasumbua wakazi, RC atoa agizo

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

JESHI la Polisi wilayani Sengerema mkoani Mwanza, limetakiwa kuimarisha ulinzi na usalama ili kuhakikisha wanawadhibiti vibaka wanaosumbua wananchi na kuhatarisha amani.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika stendi ya zamani ya mabasi pamoja na mambo mengine alilitaka Jeshi la Polisi wilayani hapa, kuhakikisha wanadhibiti vitendo vya uhalifu unaosababishwa na vibaka.

Alisema polisi wana jukumu la kusimamia usalama wa wananchi pindi unapotokea uhalifu, wanatakiwa kuchukua hatua za haraka za kuwasaka wahusika na kuhakikisha sheria inachukua mkondo wake.

"Sungusungu hawaruhusiwi kuua, kujeruhi, kumsingizia mtu kosa wala kujichukulia sheria mkononi, badala yake wanatakiwa kutoa taarifa kituo cha polisi ili wafike na kumchukua mhalifu pindi wanapokuwa wamemkamata," alisema Mtanda.

Aidha, aliwataka vijana wanaokaa vijiweni kuacha tabia hiyo bali wajikite katika kufanya kazi kwa bidii ili wapate maendeleo na siyo kubaki wanalalamika bila sababu.

Mtanda aliwataka watumishi wa serikali kuacha lugha chafu kwa jamii na badala yake wawahudumie vizuri pindi wanapofika kwenye ofisi.

# Wataka kurejea utamaduni 'shikome' kudhibiti ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

BAADHI ya wanawake na watoto katika Kata ya Mwamala Manispaa ya Shinyanga wameitaka jamii ya wasukuma kurejesha utamaduni wa kufanya vikao vya jioni vya kimaadili katika koo zao (shikome), ili kukabiliana na vitendo vya ukatili.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti na kueleza kuwa kukosekana kwa vikao hivyo kumesababisha wanawake na watoto kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na kukosa sehemu ya kusema.

Walisema vikao hivyo vilikuwa vinawapatia nafasi ya kueleza changamoto zinazowakabili na kuelimishana masuala mbalimbali ya maisha.

Mkazi wa Kijiji cha Bunonga, Ester Mandi akizungumza na Nipashe kufuatia utekelezaji wa mradi wa nafasi ya wanajamii na vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, unaotekelezwa na SPC kwa ufadhiri wa Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT), alisema kukosekana kwa vikao kumechangia kwa asilimia kubwa ongezeko la ukatili huo.

Alisema baadhi ya wazee wanakaa kwenye vijiwe vya kahawa, mabanda ya televisheni na baa mpaka saa sita usku, hawana muda wa kukaa na familia na kuzungumza nao kama ilivyokuwa miaka ya zamani.

Mkazi wa Kijiji cha Ibanza, Anna Nkinga alisema, shikome iliwasaidia wanawake kupaza sauti zao pindi wanapoonewa, hivyo kukosekana kumesababisha ongezeko la matukio ya ukatili, huku kukiwa hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kutokana na wao kukosa msaada.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwamala, Suzana Kayange alisema, utandawazi umechangia kupoteza baadhi ya mila na tamaduni za kabila hilo ambazo awali zilikuwa na faida na zilichangia kulinda maadili na kukemea wale wanaopotoka.

Akitoa takwimu za ukatili dhidi ya watoto na wanawake kwa mwaka 2019/22, Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Shinyanga, Aisha Omari, alisema mpaka kufikia Desemba mwaka 2023 wanafunzi 59 walipewa ujauzito, ubakaji 56 na ulawiti matukio tisa.

ama
ALHAMISI JUNI 13, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**Magonjwa sugu yanayotesa afya ya wazee katika maisha ya uzeeni**




**KILIMO BANGI KINAVYOATHIRI TABIANCHI... Vita vya mazingira vinavyoweka nyuma adui mkubwa zao bangi**

Ukurasa 14

## KUANGAZIA BWAWA MWALIMU NYERERE...

# Safari mwaka mmoja na nusu, agizo lake Rais kwa wizara tano

**Na Mwandishi Weti**

HADI sasa moja kati ya miradi miwili muhimu na mikubwa kitaifa inatekelezwa, ikiwamo ya umeme- Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Sehemu ya mitambo ilianzishwa na mingine ni inatarajiwa kuanza kazi karibuni, kama ilivyoahidiwa na serikali.

Ni mradi ambao ulipoanzishwa, ulikutana na hoja kinzani kuhusu hatima ya usalama wa mazingira, lakini serikali ngazi ya juu ikautolea ufafanuzi kuhusu usalama na faida zinazotarajiwa.

Baada ya kuingia uongozi wa serikali awamu ya sita, ndiyo ikachukua hatua ya uendelezaji kwa hatua zaidi hadi kufikia hatua sasa kwenye uzinduzi.

Kama ilivyo kawaida duniani kote, mfumo wa uendeshaji serikali kidunia, huendana na mamlaka za utekelezaji kisekta na maeneo maalum, ikiongozwa na safu ya mawaziri, ambako katika mfumo wa nchini wanasimamiwa na mtendaji mkuu serikalini, Waziri Mkuu.

Ni kwa mara nyingine, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaziagiza wizara tano ziazohusiana kwa karibu kisekta na Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, huku akisisitiza uhifadhi wa mazingira katika vyanzo vya maji vinayojaza Mto Rufiji, inayohusiana na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Katika orodha hiyo, Rais akazielekeza wizara za; Kilimo, Uvuvi, Maji Mazingira na Ufugaji, alipoziambia ziketi kuketi na kutumia nafasi zao Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, kupata ufanisi wake, pia umuhimu wa mto huo kimaendeleo.



Rais Dk. Samia Suluhu Hasasn, akiwa katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. **PICHA: MTANDAO.**

Ni agizo lake rais, katika tukio la kufungua ujazaji maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, akisema sekta zote zenye nafasi ya kuvuta wawekezaji na kutengeneza fursa kutokana na maji ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, zifanya hivyo, zikiwamo sekta Kilimo na Maji ambazo ni wanufaika wa moja kwa moja.

"Nazielekeza Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi na TAMISEMI na mamlaka nyingine mkapime maeneo hayo na muyaweke katika mashamba makubwa kwa ajili ya kufanya mnada wa wazi kwa wawekezaji wa uhakika katika kilimo.

"Nawasihi, pia mtenge maeneo maalum kwa ajili ya wakulima wadogowadogo hasa wa maeneo hayo yatakayokuwa na miundombinu ya umwagiliaji maji" akasema Rais Samia

Aidha, Rais akawa na maagizo yanayoilenga Wizara ya Mazingira, ambako anakufahamu vyema na alishawahi kuisimamia zamani kwa ngazi tofauti, kabla ya kuwa rais, akitaka zichukue hatua dhidi ya waharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji, mito na maeneo muhimu yanayotumika kama chanzo cha maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere

"Manufaa ya bwawa hili katika nyanja zote yanawezekana tu, kama tutatunza mazingira katika vyanzo vya mabonde ya mito inayoleta maji mabwawani. Hapa nataka nisisitize umuhimu wa 'tunza mazingira', kwani huu mradi tumeujenga kwa gharama kubwa na kwa kujinyima vitu vingi muhimu.

"Itakuwa ni dhambi kubwa kama hautatimiza malengo yake kwa sababu ya uzembe na ubinafsi wetu kwahiyo kulinda mazingira na kulinda mradi huu sasa ni suala la kufa na kupona," akatamka Rais Dk. Samia

Ni katika nafasi hiyo, aliyekuwa Waziri wa Nishati wakati huo, January Makamba, pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi wa shirika la umeme, TANESCO Maharage Chande, akasema serikali inaendelea na mipango ya muda ya mrefu ya kukabiliana na changamoto ya umeme.

Hapo katika orodha hiyo inajumuisha kujengwa mabwawa manne pamoja na kuanzisha miradi mingine kupitia nishati jadilifu, ili kukabiliana na changamoto ya umeme.

"Tupo katika kupanga mbele na ukiangalia ile chati yetu sisi leo hii tunajua mpaka 2040 mradi gani utaingia kwenye gridi, tumejipanga kwa muda mrefu na sio kwa muda mfupi, tunachoomba ni subira tatizo la kukatika umeme litaisha..." alisema.

Hadi sasa, ni wastani wa mwaka mmoja na nusu tangu agizo lake Rais Dk. Samia, picha ya kazi za mjumuiko unapaswa kuanikwa kwa umma kilichofanyika, kuhusiana na fahari yao umma; Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Eneo mojawapo mahsusi katika utekelezaji agizo hilo la Rais, linasimama katika mazingira na manufaa ya kiuchumi, kazi inayopaswa kufanyika kutoka kwa wataalamu wa kiwizara na serikali kwa upana wake, hata inapobidi inavuka mchango wa nje ya serikali.

MAZINGIRA

# USAID, wadau mazingira wanavyorudisha ushoroba wa Nyerere-Selous-Udzungwa

**Na Jenifer Gilla**

USHOROBA wa Nyerere-Selous-Udzungwa ni moja ya maeneo muhimu ya kijiografia na kiikolojia nchini Tanzania. Ukiunganisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere (Selous) na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa, ambapo wanyama hutumia kama njia wakielekea kutoka hifadhi moja kwenda nyingine.

Kutokana na hali hiyo, imekuwa sehemu muhimu ya vivutio vya utalii na kuwanufaisha wakazi wanaozuka na fursa zipatikanazo ikiwamo utalii.

Kwa umuhimu wa eneo hilo, serikali ilichagua kati ya shoroba 20 ambazo za kuzihifadhi, ili kuwanufaisha wananchi wa eneo hilo na waone umuhimu wa kuwapo rasilimali hiyo na washiriki kuihifadhi.

Mkurugenzi wa Wanyamapori wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Fortunata Msofe, anasema ni ushoroba unaokabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukataji miti unaofanywa na wanavijiji jirani na migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Hata hivyo, ushoroba huu unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukatwaji wa miti unaofanywa na wanavijiji waouzunguka eneo hilo, na migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Akizungumza na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa, Theodora Batiho, anasema pamoja na juhudi wanazochukua kutoa elimu kwa jamii kuhifadhi ushoroba huo, tatizo bado linaendelea, sababu kuu ikiwa ni uhitaji wa nishati ya kupikia.

Anakiri pia wanyamapori waharibifu kama vile tembo kuvamia makazi ya watu wakati wakivuka kutoka hifadhi moja kwenda nyingine, na kusababisha uharibifu wa mali za wanakijiji na kuleta taharuki.

"Shughuli hizi za kibinadamu zimeathiri sana uwezo wa ushoroba huu katika kusaidia uhamaji wa wanyamapori na kuhifadhi bayoanuai," anasema.



Meneja Programu wa Asasi ya Reforest Africa, Lasima Nzao,akiwaonyesha kitalu cha kuzalisha miti ya asili wanachokiratibu . **PICHA: JENIFER GILLA**

Kwa kuiona changamoto hiyo, na lengo la serikali la kurudisha hadhi yake, Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) kupitia Mradi wa Tuhifadhi Maliasili kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi waliamua kuongeza nguvu kurejesha misitu katika ushoroba huo wakishirikiana na wanavijiji.

Kurejesha ushoroba

Lasima Nzao, ni Meneja Programu wa Asasi ya Reforest Africa, anasema USAID-Tuhifadhi Maliasili wamewezesha kupanda miti ya asili katika eneo la Msitu wa Hifadhi Asili wa Magombela, ambao ushoroba wa Nyerere-Selous-Udzungwa unapita.

Anasema kupitia mradi huo wamekwenda msituni kutafuta mbegu na kuzichanganya, kuziotesha kwenye vitalu na miti ikishakuwa wanaipanda katika eneo hilo kwa kushirikiana na wanakijiji.

Katika mradi huo wa miaka miwili, Reforest imedhamiria kupanda miti 100,000 na mategemeo ni mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi huu, wanatakuwa wamepanda miti 50,000 japokuwa wanakabiliwa na changamoto ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Miti hii itasaidia kupendezesha ushoroba na kuweka mazingira rafiki kwa wanyamapori kupita hivyo kumaliza tatizo la wanyamapori kuvamia makazi ya watu na kufanya uharibifu," alisema.

Pia shirika linawapa wanavijiji elimu ya namna ya kunufaika na misitu hiyo na kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile ufugaji nyuki.

Katika kuhakikisha kuwa usimamizi wa rasilimali misitu unafanywa na wanakijiji wenyewe kwa weledi USAID-Maliasili inashirikiana na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA), kuanzisha programu utawala bora katika urejeshaji wa ushoroba huo kwa kutumia mfumo wa Pima Kadi.

Ofisa Mradi wa USAID, Tuhifadhi Maliasili-MJUMITA, Kelvin Shirima, anasema programu hiyo wanaitekeleza katika vikundi kwenye mitandao 129 iliyopo katika kanda sita, mikoa 14, wilaya 32, na vijiji zaidi ya 452.

Anaulekezea mfumo wa Pima Kadi, kuwajibikaji wa viongozi katika vikundi vinavyojihusisha na urejelezaji wa ushoroba huo katika vijiji vinavyozunguka shoroba hiyo kama vile Sole, Mang'ula A, na Kanyenja.

Kupitia programu hiyo wametoa mafunzo ya ufuatiliaji kwa kwa watu zaidi ya 50 na kuwapa fomu zenye alama za ubora ambazo wanatumia kujipima uwajibikaji wao na yule atakayepata alama za chini wanampa mbinu za kujiboresha na kama tatizo hilo mlitajirudia mara kwa mara anaweza kukosa sifa ya kuendelea.

Anasema mpango huo unalenga jamii inawajibika kutunza rasilimali zake kwa maendeleo endelevu kwa manufaa yao wenyewe kwani uharibifu wa shoroba ni hatari kwa wanyamapori na hata wanakijiji.

Anataja changamoto zinazosababishwa na wanajijiji wenyewe kuwa ni ukataji miti bila utaratibu maalum, uwindaji haramu, kilimo katika eneo la hifadhi na uchafuzi wa vyanzo vya maji jambo linaloathiri jambo linaloathiri ushoroba na ustawi wa bayoanuai.

Anasema kupitia programu hiyo wamefanikiwa kuimarisha ulinzi wa mipaka, kutoa elimu kwa jamii kuhusu uhuhimu wa kuhifadhi rasilimali hiyo na mwamko wa wanavijiji kulinda eneo hilo bila kusukumwa na kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

**ELIMU KWA JAMII**

Mratibu wa Programu wa Shirika la Associazione Mazingira, Felister Mwalongo, anasema kupitia mradi huo wanatoa elimu ya uhifadhi wa mazingira katika vijiji vinavyozunguka hifadhi ili wawe mstari wa mbele kuitunza kwa manufaa yao wenyewe.

Anasema, pia wanatoa elimu hiyo katika shule za msingi na kupitia mradi huo wamesahawafikia wanafunzi 300 na walimu 45 na kugawa miche ya miti 60,000 ndani ya miezi minne.

Mkuu wa Uhifadhi wa Hifadhi Milima ya Udzungwa, Theodora Aloyce, anaisema kuwapo wa shoroba ni muhimu, kwa sababu kunasaidia wanyama kwenda sehemu nyinginezo na kuzaliana hivyo kuepusha wanyama wa aina moja kuzaliana pamoja na kupunguza maambukizi ya magonjwa.

Anawashukuru USAID-Tuhifadhi Mazingira kwa kazi kubwa ya kufadhili wadau wa mazingira katika eneo hilo ili kurejesha hadhi ya shoroba hiyo, kwani umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto zilizokuwapo ikiwamo migongano baina ya binadamu na wanyama.

Shoroba hiyo yenye urefu wa kilomita 13 inapita katika vijiji vya Sole, Kanyeja na Mang'ula A na inaunganisha Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

# Ilivyo vita kusaidia watoto wenye jinsi mbili

**Na Yasmine Protace**

MTOTO kuzaliwa na jinsi mbili ni hali ambayo mtu kuzaliwa na jinsia ya kiume au ya kike. Hapo jinsia zote zinaweza kuwa sehemu moja au sehemu tofauti.

Kimsingi, mwonekano wa nje huwa haueleweki, kwa urahisi kiwango cha mwonekano wa nje wa jinsia hizo hutegemea kwa kiwango cha homoni iitwayo' tosterone' inayozalishwa kuanzia wiki ya nane mpaka ya 11 baada ya mimba kutungishwa.

Hivyo, hapo jamii hutakiwa kitaalamu, wasiwafiche watoto hao majumbani na badala yake wafikishwe hospitali, ili waweze kupatiwa matibabu.

Inawezekana jamii haina elimu ya jinsia mbili na hivyo mtoto anapozaliwa huonekana kama ni mkosi na kuamua kumficha.

Ukosefu wa elimu kwa wazazi ni moja ya changamoto inayochangia baadhi ya walezi na wazazi kuwanyima haki zao za msingi watoto wanaozaliwa na jinsi mbili.

Kuzaliwa kwa mtoto kuwa na jinsi mbili, baadhi ya wazazi wanatajwa kuwaficha watoto hao, ili wasiweze kutambulika.

Kutokana na kuwaficha watoto hao, serikali sasa inatoa huduma kwa watoto hao na kuwataka wazazi kutowaficha watoto hao na badala yake, wafikishwe katika vituo vya afya.

Kuwaficha watoto hao ni kuwanyima haki zao za msingi. Hivyo, serikali inawahakikishia wazazi tatizo la jinsia mbili linatibika.

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anasema kuwa anatoa wito kwa Watanzania kuacha tabia ya kuwaficha watoto wenye jinsi mbili bali wawapeleke hospitali ili waweze kupata huduma mapema kwa kuwa tatizo hilo linatibika.

Waziri Ummy amesema hayo wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Tatu wa Chama cha Madaktari wa Upasuaji Urolojia Tanzania (TAUS) unaofanyika Jijini Dar Es Salaam.

"Wazazi/Walezi msiwaficha watoto wanaozaliwa na jinsi mbili bali muwapeleke mapema hospitali ili waweze kupata matibabu mapema kwa kuwa tatizo hilo linatibika, lakini pia sio aibu kuzaliwa katika hali hiyo," anasema.

Anasema, mtoto anaweza kufanyiwa upasuaji mapema, akapimwa na akagundulika kuwa yeye ni wa jinsi gani, sio hadi mtoto anakua hajijui yeye ni wa jinsi gani kama ni mwanamke au mwanaume.

Aidha, Waziri Ummy amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha matibabu katika

Inaendelea Uk. 14

AFYA

# Magonjwa sugu yanayotesa afya ya wazee katika maisha ya uzeeni

**Na Flora Wingia**



Mzee akipata tiba kliniki. **PICHA: MTANDAO**

AFYA ya wazee na uzee, ni moja ya maeneo yanayotiliwa mkazo sehemu mbalimbali duniani, kutokana na kuwa na magonjwa sugu yanayosumbua kundi hilo maishani.

Mtaalamu na Mshauri wa Masuala ya Afya ya Jamii, Dk. Ali Mzige, anafafanua kwamba inakadiriwa watu milioni moja, wanavuka kuingia umri miaka 60, kila mwezi duniani.

Anataja karne ya 20 inaingia na ongezeko la wazee katika nchi zinazoendelea na zilizoendelea. Inakadiriwa katika robo ya karne ya 21, idadi ya wazee duniani itakuwa na mitazamo kadhaa.

Inatajwa, miaka mitano baada ya 2020, Wajapani watakuwa na idadi kubwa ya wazee duniani, kwa asilimia 31 watakuwa na umri zaidi ya miaka 60, wakifuatiwa na Italia, Ugiriki na Uswisi.

Kadhalika, inakadiriwa kuvuka miaka hiyo, nchi tano kati ya 10 zenye idadi kubwa ya wazee zitakuwa: China, India, Indonesia, Brazil na Pakistan.

Ikaelezwa kuwa ifikapo mwaka 2020, inakadiriwa idadi ya wazee katika nchi zinazoendelea, itaongezeka kwa kiwango asilimia 240, kutoka iliyokuwapo miaka ya 1980; sababu ni kupungua watoto wanaozaliwa na ongezeko la umri wa kuishi.

Kitaalamu inafafanuliwa kusababisha na kuwapo teknolojia iliyoendelea, zikiwamo dawa za kutibu magonjwa mbalimbali.

Wanawake kwa wastani wanatajwa wanaishi muda mrefu, kuliko wanaume takriban katika kila nchi. Idadi ni kubwa iko katika kundi la wazee na wajane, huku wazee hao ndio watoa huduma kwa wazee wenzao duniani.

### HALI YA TANZANIA

Tanzania inakadiriwa kuwa na wazee milioni 3.5 au zaidi, wenye umri kati ya miaka 60 na 65 na idadi yao inaongezeka kila mwaka.

Magonjwa sugu yanayowasibu wazee duniani kote ikiwamo Tanzania: Magonjwa ya moyo, ikiwamo shinikizo la juu la damu- presha pia saratani (kansa) za aina mbalimbali, kama mapafu, kibofu cha mkojo, tezi dume (prostate), pia shingo la mfuko wa kizazi kwa wanawake.

Dk. Mzige anasisitiza kuwa ugonjwa wa kisukari kwa anayeugua ni wa maisha, pia presha, akifafanua nasaha yake vijana wasidanganywe na wale wanaojinadi kuyatibu.

"Nimeujua ugonjwa wa kisukari na presha miaka 50 iliyopita nikiwa shule ya sekondari. Hadi leo, presha na kisukari kinadhibitiwa, ili mgonjwa asipate matatizo ya muda mrefu," anafafanua Dk. Mzige.

Anasimulia karaha watu walizopata kwa kunywa kilichoitwa 'Kikombe cha Babu' kukabili magonwa yao.

Pia, anataja magonjwa mengine yanayowatesa wazee ni ya viungo na nyonga (osteoarthrosis and hip joints), hasa wanapokuwa na uzito mkubwa zaidi ya kilo 70 kwa mwanaume na 60 kwa mwanamke.

"Endapo katika ujana na usichana wako hukushiriki michezo, wala kupiga kwata, pia hukubahatika kwenda Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ulikaa ukaponda raha, shida itakupata," anasema.

Dk. Mzige anasema, mtu anapofanya mazoezi ya viungo mwilini, asiache endelee na kama Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili (marehemu), Mzee Ali Hassan Mwinyi.

"Huyu alikuwa kigezo changu cha 'mzee na uzee', lakini sio ugonjwa, bali maumbile. Magonjwa ya mapafu ikiwamo kifua kikuu na mengine yanasababishwa na uvutaji wa sigara.

"Magonjwa ya akili hususan kupoteza kumbukumbu, upweke na wasiwasi wa ziada (anxiety), msongo wa mawazo (stress) na sononа, kiharusi (stroke), husababishwa na shinikizo la damu," anasema.

Anasema, pia maradhi ya Ukimwi yanasababisha kiharusi, hasa kwa wasio na presha au kisukari, akiorodhesha pia, uvutaji sigara na unywaji pombe kupindukia, nazo ni wakala wanaowezesha kiharusi.

Dk. Mzige anatahadharisha kuwa mtu asipokunywa maji ya kutosha, akipoteza maji mengi ama kwa njia za jasho na mkojo, anaweza kupata maradhi kiharusi, akitoa elimu ya uwiano anapokufa Mwingereza

> "Endapo katika ujana na usichana wako hukushiriki michezo, wala kupiga kwata, pia hukubahatika kwenda Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ulikaa ukaponda raha, shida itakupata," anasema.

mmoja kwa kiharusi London au kokote nchini kwao, Tanzania kunakuwapo vifo kama hivyo 10.

Mtaalamu huyo anafafanua, hiyo inatokana na imani anayoinukuu akimtaka: "Mwenye kiharusi karogwa au amechezewa mpelekeni kwa... (fundi-mganga wa jadi) ..."

### MAGONJWA MACHO

Eneo lingine analitaja ni magonjwa ya macho na hasa 'mtoto wa jicho' au trakoma, ambao unapokosa usahihi wake, unaweza kumpatia upofu wa macho.

Vilevile, Dk. Mzige anataja shida ya presha ya macho (glaucoma) ambayo ikipanda sana, inahatarisha uono wa mtu, akinena ni tatizo la wazee wa jinsia zote kutokana na umri, wengine upungufu wa lishe zao.

"Kama hilo miwani ipo inasaidia kurekebisha, kushindwa kusikia vizuri, hatua inapofikia hapo ni kumuona Daktari wa Pua, Koo na Masikio, ili upime na ikibidi upatiwe kifaa kitakachokusaidia kusikia," anasema Dk Mzige.

Anaitaja kadhia nyingine ya wazee na uzee wao, ni kupoteza meno kuwa kibogoyo, akitoa tahadhari hiyo ngumu iakuwapo kwa mgonjwa asiye na huduma za Bima ya Afya, kumhudumia.

Hapo mtaalamu huyo anatumia uzoefu wake, akishauri kuwa, ni vema wazee wasiokuwa na Bima ya Afya, wapewe mfumo wa tiba kwa kadi, au Mfuko wa Afya wa Jamii, utakuwa ukombozi wao wa kudumu.

Binafsi, anasema utumishi wa umma miaka 11 iliyopita na amekuwa akipewa somo la kufundisha afya za wazee wanapokaribia kustaafu, au kwa waliokwishastaafu.

Mafunzo hayo, anasema anayatoa kwa watumishi wanaoanza ajira, ili wajiandae kuwa na afya nzuri, wakiwa kazini kabla hawajastaafu.

### MAGONJWA AKILI

Magonjwa ya akili yamo katika kundi la magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Hofu na wasiwasi, ni kitu cha kawaida katika maisha, lakini inatajwa inapozidi, huathiri maisha ya mhusika ya kila siku.

Kazi nyingi, zinatakwa kuleta matatizo ya malezi ya watoto na wajukuu au vilembwe, ndoa inayoyumba, kufukuzwa kazi, gari kuharibika, kukosa fedha za kulitengeneza.

Wahusika ni wengi, na wanaonekana kabla ya kustaafu au baada ya hapo, walikuwa wanahitaji huduma za tiba uzeeni (geriatric medicine) na kwa bahati mbaya wanazikosa.

Hapo kunatajwa haja ya kuanzisha huduma aina hizo; ushauri nasaha na maelekezo ya cha kufanya, anapopata tatizo la magonjwa ya akili.

Ana ufafanuzi mwingine, baadhi ya wazee wanakosa mlo kamili, hali inayosababisha kuwa na lishe duni, huku kukiwapo asilimia 20 ya wagonjwa wa akili wanaolazwa wodini katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, wameathirika na ulevi wa pombe na dawa za kulevya kwa vijana wetu.

***Kwa ushauri zaidi wasiliana kupitia amzige@hotmail.com au simu: 0713 410 531.***

MAZINGIRA

## KILIMO BANGI KINAVYOATHIRI TABIANCHI...

# Vita vya mazingira vinavyoweka nyuma adui mkubwa zao bangi

## •Mpiganaji pekee Mamlaka Udhibiti, yafyeka ekari 2,389

**Na Zanura Mollel**




Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo. **PICHA: ZANURA MOLLEL.**

INAPOTAJWA bangi, katika mustakabali mpana unagusa wengi, mazingira hadi tafsiri ya upatikanaji wake, kuanzia afya ya jamii, hadi inavyoharibu mazingira, tabianchi hata kuitikisa dunia, hasa ikichangiwa na mfumo wa upatikanaji wake.

Imo katika dawa za kulevya zilizopigwa marufuku nchini. Kilimo chake na athari inawagusa wakulima, wanaofyeka misitu na mapori, wanalima pembezoni mwa vyanzo vya maji. Kwa ujumla hakuna uhalali nchini.

Taarifa ya Kamishna Jenerali Aretas Lyimo, wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) ya Aprili 4 mwaka huu, inabainisha kuwapo mashamba makubwa ya bangi katika hifadhi za msitu ya Ubangu mkoani Shinyanga na Mabatini mkoani Tabora.

Anafafanua: "Kwa ushirikiano kutoka kwa Wakala wa Misitu (TFS), tulifanikiwa kuteketeza mashamba hayo na kuwakamata wahusika."

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka 2022 inasema matumizi ya nishati chafu kwa ajili ya kujitegemea, ambayo kuna watu bilioni 2.4 walionekana kutumia nishati hiyo, wanaopoteza hekta 3.9... za misitu kupotea kila mwaka barani Afrika.

### RIPOTI DCEA,2023

Ripoti ya DCEA mwaka jana, inaeleza kimazingira matumizi ya dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano, husababisha uchafuzi wa mazingira, pale vifaa vya kujidunga kama sindano huweza kuwa na vimelea vya maradhi zinapotupwa kwenye vichochoro, viwanja vya michezo, fukwe na vituo vya daladala.

Ripoti inaeleza kilimo cha bangi huharibu mazingira kwa kusababisha ukataji miti misituni na kuharibu vyanzo vya maji. Watumiaji dawa za kulevya, wanatajwa kuchafua hewa kwa moshi, wakiwadhuru kiafya watu jirani.

Kudhibiti kilimo hicho, ripoti hiyo inasema kulifanyika uteketezaji wa ekari 2,389 za mashamba ya bangi katika mikoa ya Arusha, Morogoro na Mara, magunia 251 ya mbegu za bangi zilikamatwa na kuteketezwa katika mikoa ya Arusha, Morogoro na Mara.

Ripoti ya Dunia ya Dawa za Kulevya mwaka jana, iliyozinduliwa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC), imezungumzia ulanguzi wa dawa za kulevya na uhalifu unaoathiri mazingira katika Bonde la Amazon Kusini mwa Amerika na sehemu za majaribio ya kitabibu yanayohusisha dawa hizo kuovuruga akili.

### WADAU MAZINGIRA

Mkurugenzi wa Taasisi ya NOTA KA TZ inayojishughulisha na Uhifadhi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Careen Mwakitalu, anasema walimaji bangi wanachangia uharibifu wa mazingira na kuchochea mabadiliko ya tabianchi, kutokana na kilimo hicho kufanyika kwa siri.

"Wanalima pembezoni mwa vyanzo vya maji, wanachangia mvua kunyesha nyingi na wakati mwingine kidogo pamoja na mabadiliko ya misimu ya mvua. Hii ni kutokana na kipindi cha maandalizi uchoma na kufyeka maeneo moshi kutokana na uchomaji taka mashambani unaathiri uso wa dunia," anasema Mwakitalu.

Anafafanua, kwa uso wa dunia (ozone layer) unapotoboka kutokana na moshi, ndio inachangia kuongezeka joto duniani, kuwapo jua kali na kusababisha mazao shambani kuathirika, hata kuchochea ukame wa muda mrefu duniani.

"Kilimo hicho (cha bangi) kinachangia rutuba ya mchanga na wadudu hai kufa kutokana na uchomaji wa taka au mkaa wakati wa maandalizi ya mashamba ya bangi," anasema Mwakitalu.

Mkurugenzi wa Muunganiko wa Mashirika ya Mabadiliko ya Tabianchi zaidi ya 50 nchini, Faraja Emily, anaeleza mabadiliko ya tabianchi yameshawaathiri vijana wengi na kujihusisha katika matumizi, biashara na kilimo haramu cha bangi, ikiendana na tatizo la afya ya akili, kutokana na changamoto ya ajira.

"Kundi kubwa la vijana katika kata ya Ubungo eneo la Kibululu huko Goba (Dar es Salaam) wamejiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya baada ya eneo la Mto Mbezi walilokuwa wakifanya shughuli za ukusanyaji mchanga kuathiriwa na mvua zilizonyesha 'haya ni matokeo ya mabadiliko tabiachi'...

"Tupo tayari kushirikiana na mamlaka husika katika kuweka mkakati wa kupunguza uharibifu wa mazingira kupitia kilimo cha mmea huo kwa kukutanisha vijana ambao ndio kundi kubwa linalotajwa kujihusisha na matumizi ya dawa hizo;zaidi nikuwekeza nguvu katika kutoa elimu," anasema Emily.

Mkuu wa Mawasiliano na Uchechemuzi wa Asasi ya Plan International, Sesilia Bosco, anafafanua "athari yake (kiafya na kimazingira) huonekana kwa kipindi cha miaka mitano hadi kumi. Wananchi hawana uelewa elimu inahitajika zaidi.

"Moshi wa bangi uchangia magonjwa mbalimbali ikiwamo wa mapafu, kifua na hata sasa ukifuatilia kunaongezeko kubwa la magonjwa yanayotokana na mfumo wa hewa, "anasema Bosco.

### HALI ILIVYO

Ripoti ya Dawa za kulevya mwaka 2023, inaonyesha ongezeko la watumiaji dawa hizo kwa watu 11,608 kipindi cha miaka sita, serikali inaendelea kuwapatia matibabu katika vituo vya kutoa huduma (MAT), ikifafanuliwa:

"Mwaka 2023 idadi ya waraibu ilikuwa 15,915 mwaka 2022 ni 13,619 lakini mwaka 2017 waraibu waliosajiliwa katika vituo vya kutolea huduma walikuwa 4,307".

"Kupitia ripoti hiyo ni dhahiri kuwa uchafuzi wa mazingira unaongezeka kupitia wazalishaji na watumiaji wa dawa za kulevya, mikoa mitatu inayoongoza kwa matumzi ya dawa hizo mwaka 2023 ni Dar es Salaam waraibu 10,829 Tanga 1,302 na Pwani 1,219 hao ni waliosajiliwa katika vituo vya matibabu(MAT," unafafanua uchambuzi.

Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini(TARI), Dk. Deusdedith Mbanzibwa, anasema kupitia sayansi ya mimea na udongo, kuchoma moto wakati wa maandalizi ya mashamba kwa ajili ya kilimo kunachangia uwezo wa udongo kushindwa kushikilia maji pamoja na kuua viumbe rafiki ambavyo huitajika kwa ajili ya kurutubisha udongo na kuwezesha mimea kuota kwa afya.

Hata hivyo, imebainika katika ufuatiliaji wa Nipashe, umekosekana utafiti kuhusu kilimo cha mmea wa bangi hapa nchini, kwa mashirika mengi yanayojishughulisha na utunzaji mazingira na mabadiliko ya tabianchi, ikikosa mpango mkakati wa kutoa elimu ya athari za dawa za kulevya kimazingira.

# Ilivyo vita kusaidia watoto wenye jinsi mbili

**Inatoka Uk. 12**

nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na kuwa nchi ya kutembelewa kwa ajili ya tiba utalii.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameanzisha programu maalumu iitwayo Dk. Samia Super-Specialized Scholarship Program ya ufadhili wa wataalamu wa ubingwa bobezi ambapo katika mwaka wa masomo 2023/2024, jumla ya Shilingi bilioni 10.9 zilitengwa kwa ajili ya ufadhili wa wanafunzi 1,109 kwa ajili ya masomo ya ubingwa na ubingwa bobezia," anesema Waziri Ummy.

Anafafanua, kati ya wanafunzi hao 1,109 wanafunzi 33 watakwenda kusomea ubingwa bobezi kwa ongezeko la wanafunzi 26 sawa na asilimia 37 ikilinganishwa na mwaka wa masomo wa 2022/2023 ambapo kulikuwa na wanafunzi 7 wa ubingwa bobezi.

"Kulingana na ufadhili wa programu hii, jumla ya wanafunzi 48 wanasomea udaktari bingwa wa upasuaji urolojia na kati yao madaktari 5 wanasomea ubingwa bobezi wa upasuaji urolojia." anasema.

Kwa upande wake rais wa Chama cha madaktari wa upasuaji Urolojia Tanzania (TAUS) Prof. Sydney Yongolo, anatoa wito kwa madaktari vijana kujiendeleza kimasomo katika fani za ubingwa bobevu kwa kuwa Serikali inaendelea kuweka mazingira rafiki katika utendaji kazi ikiwemo kuwatambua madaktari bingwa.

"Tunaendelea kuwasisitiza madaktari kujiendeleza kimasomo hasa kutumia fursa ya programu maalumu iitwayo 'Dk. Samia Super-Specialized Scholarship Program' ya ufadhili wa wataalam wa ubingwa bobezi iliyoanzishwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan," anasema.



# VETA yajivunia mafanikio miaka mitatu ya Rais Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMLAKA ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) Kanda imepokea zaidi ya Shilingi bilioni 7.7 kukamilisha ujenzi wa vyuo vitatu katika wilaya za Kongwa Chemba na Bahi mkoani hapa, imefahamika.

Hayo yalisema juzi jijini hapa na Kaimu Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Kati, Ramadhani Mataka wakati akizungumzia mafanikio ya mamlaka hiyo katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio hayo yaliyopatika katika kipindi cha uongozi huo wa serikali ya awamu ya sita, alisema Rais Samia ameiwezesha VETA Kati kukamilisha ujenzi wa vyuo hivyo ngazi ya wilaya ili kutimiza azima yake ya kuhakikisha wilaya na mikoa nchini zinakuwa na vyuo vya ufundi na kuwawezesha vijana wengi zaidi kujiunga na mafunzo ya ufundi.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo vipya 64 vya ufundi kwenye wilaya nyingine nchini ikiwamo Mpwapwa, Kondoa na Chamwino za kanda hiyo ya Kati kwa gharama ya zaidi ya Shilingi bilioni 4.2.

"VETA Kanda ya Kati mahitaji yetu ni kutoa wanafunzi bora na siyo sifa ya kuwa na vyuo vingi ambavyo vijana wake hawakubariki na jamii. Kufanikisha kwa vyuo hivyo, vijana wanategemea watakuwa na ujuzi na maarifa ya kufanya kazi, alisema.

Alisema ili kuwawezesha vijana hao wakiwamo wanawake na wajasirimali kuwa sehemu ya nguvu kazi nchini, mamlaka hiyo itaendelea kujikita kwenye miradi itakayowawezesha kujiajiri kwa kupatiwa mafunzo ya stadi za ujasiriamali na usimamizi wa miradi ya kiuchumi na kuwawezesha kurasimisha shughuli zao.

Hata hivyo, Mataka alisema Veta imejipanga kuwasaidia wakulima wa zao la zabibu na alizeti kwa kuwapa elimu ya ufundi stadi kwenye uchakataji wa mvinyo na mashine za kukamua.

# RC: Wazazi wanaotishia kuua walimu wakamatwe

**Na Thobias Mwanakatwe,**

IRAMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida, limeagizwa kuwasaka na kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wazazi wanaodaiwa kuwatishia kuwaua baadhi ya walimu wa Shule ya Sekondari Mtekente wilayani hapa kwa kuwaadhibu watoto wao kwa utovu wa nidhamu.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa huo, Halima Dendego, baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa walimu hao kuwa wanaishi kwa hofu na kukosa amani baada ya kupokea vitisho kutoka kwa wazazi hao. Walimu hao walitoa madai hayo juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego baada ya kufika shule hiyo kukagua ujenzi wa mabweni uliogharimu Sh.milioni 180 kwa ufadhili wa kiwanda cha kuchambua pamba cha Biosustain.

"Kuna siku tukiwa ndani tulisikia kishindo kikubwa, tulipotoka nje tukakuta madirisha mawili yamepigwa mawe na mlangoni ujumbe unamtaja mwalimu mwenzetu kumweleza kuwa tutakuua wewe na wenzako kwa tabia ya kuwaadhibu wanafunzi," alidai Mwalimu Ramadhani Mkuga.

Mwalimu Mkuga, alidai kitendo cha kutishia kuuawa kwa kuwaadhibu wanafunzi kwa utovu wa nidhamu ni kuwazuia walimu hao kutekeleza majukumu yao na kuwajenga wanafunzi katika maadili mema.

Alidai baada ya kutishiwa kuawa walitoa taarifa kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na kwamba hadi sasa wazazi hao waliotoa vitisho hawajapatikana.

"Hapa tunaishi kwa mashaka makubwa kwa sababu hatujui nini kitafuata, hakuna hatua zozote kwa hiyo siku moja wanaweza kuja kufanya kweli, " alidai.

Baada ya kupokea madai hayo, Dendego, alitaka kitendo cha wazazi kuzua hofu kwa walimu na kuwakosesha amani kiwe mwisho.

Aliwataka wakazi wa kijiji hicho kwenda kuwaeleza vijana wao likitokea jambo lolote linalohatarisha maisha ya walimu hao, serikali itachukua hatua kali dhidi yao.

"Mkuu wa Kituo cha Polisi usitake mimi nije kufanya kazi yako hapana hapana, ukitaka kukamata mhalifu wewe ni dakika moja tu sababu umefundishwa kazi hiyo, mkitaka mimi nifanye nitafanya na nitaweza, lakini ninyi itabidi mtupishe, " alisema Mkuu huyo wa mkoa.

Aliagiza atakapokwenda kuzindua mabweni ya shule hiyo akute watuhumiwa wote wamekamatwa na kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka dhidi yao.

"Nimemwagiza kamanda (Mkuu wa Kituo), RPC (Kamanda wa Polisi Mkoa, Amon Kakwale) na OCD (Mkuu wa Polisi Wilaya haitakiwi eneo lolote la nchi hii ya Tanzania ukiwamo Mkoa wa Singida watu wanakosa amani," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa, pia alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kuhakikisha mabweni hayo yanafanyiwa marekebisho ya dosari zilizopo katika maeneo machache.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akitoa ufafanuzi kuhusu madeni ya baadhi ya watumishi wanayoidai serikali, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chuo cha Mipango, Maendeleo Vijijini chajiongeza kidijitali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO Cha Mipango na Maendeleo Vijijini (IRDP) kimeanza kutumia mfumo wa kielektroniki kufundishia ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuwafikia wanafunzi wengi ndani na nje ya nchi kujiendeleza kielimu.

Makamu Mkuu wa Taaluma, Utafiti na Ushauri Elekezi wa IRDP, Profesa Provident Dimoso, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya kufundishia kwa wahadhiri na wataalamu wengine wa chuo hicho.

Profesa Dimoso, alisema mfumo huo utasaidia kupunguza mzigo kwa wahadhiri, kuongeza ufanisi, idadi ya wanafunzi na kuongeza mapato ya chuo.

Alisema kwa sasa mahitaji ya wanafunzi kujiunga na chuo hicho yameongezeka, hivyo kupitia mfumo huo watawafikia watu wengi zaidi ndani na nje ya nchi.

"Watu wengi hivi sasa wanatamani kusoma, lakini mtu hawezi kuomba likizo ya mwaka mzima ili kuja kusoma chuoni, wengi wanataka kusoma wakiwa kazini, hivyo mfumo huu utakiwezesha chuo kupata wanafunzi wengi na kuwahudumia popote walipo bila shida yoyote," alisema na kuongeza:

"Mfumo huu unaweza kumuhudumia mwanafunzi popote akiwa Kenya, Burundi au hapa nchini ambako hatuna kampasi, mwanafunzi anaweza kupata vipindi, kumuuliza maswali mwalimu wake, pia kupitia video ambazo zinawekwa kwenye mfumo anaweza kujifunza zaidi, kufanya majadiliano na wanafunzi wenzake kutoka maeneo mengine," alisema.

Kwa mujibu wa Profesa Dimosso, mfumo huo utakipunguzia chuo hicho gharama za uendeshaji kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi kusoma badala ya kujisajili chuoni.

"Kupitia mfumo huu wanafunzi wengi watasoma kule waliko hakuna haja ya kuja chuoni hii itasaidia kupunguza gharama za chuo kuhudumia wanafunzi wake, uwekezaji wa fedha nyingi kwenye ujenzi wa majengo na kukiongezea chuo mapato," alisema.

Alisema kupitia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha matumizi ya teknolojia kufundishia, chuo hicho kitasaidia watumishi wengi waliko kazini kujiendeleza kielimu.

"Kwa miaka mitano hapa Dodoma chuo tumejenga majengo kwa ajili ya madarasa, ofisi. Kampasi ya Mwanza tumehama kwenye jengo la kupanga, tumekuja kwenye majengo yetu, lakini wanafunzi bado wanaongezeka kila mwaka na wengi ni watumishi hasa hapa makao makuu, mfumo huu utasaidia kuwahudumia," alisema.



# Maofisa halmashauri wadaiwa kuvamia nyumba, kudai ushuru

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa vijiji vya Isinura na Ikanutwa wilayani Mbarali mkoani Mbeya, wamewalalamikia watoza ushuru wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kuvamia ndani ya nyumba zao na kuwalazimisha kulipa ushuru wa mazao ambayo wamejiwekea akiba kwa ajili ya chakula.

Wakizungumza na Nipashe wakulima hao walisema hali hiyo imeanza kuhatarisha amani kwenye vijiji vyao kutokana na wananchi kugoma kulipa ushuru huo na hivyo kusababisha ugomvi baina yao na watoza ushuru hao.

Alphonce Matagri ambaye ni mkulima wa Kijiji cha Ikanutwa alisema juzi watoza ushuru hao wakiwa na gari la halmashauri walifika nyumbani kwa mmoja wa wakulima wa kijiji hicho na kumtaka afungue nyumba yake ili wahesabu magunia ya mpunga aliyojiwekea akiba kwa lengo la kuyalipia ushuru.

Alisema mkulima huyo alikataa kufungua nyumba na watoza ushuru hao wakaanza kumlazimisha na ndipo mkulima huyo akaanza kupiga mayowe ya kuomba msaada.

Alisema kuwa baada ya wananchi kufika eneo la tukio walianza kuwashambulia watoza ushuru hao kwa kuwapiga mithiri ya wezi mpaka alipofika Mwenyekiti wa Kijiji na kuwaamuru waache.

"Kama sio mwenyekiti wa kijiji kuwazuia wananchi wangewaua watu wale na pengine hata gari lingechomwa moto, kwa kweli amani ilianza kutoweka kabisa," alisema Matagri.

Alisema baada ya mwenyekiti kuwanusuru watoza ushuru hao waliondoka na baadaye walishangaa kuona askari polisi wakifika kijijini hapo na kuwakamata Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji na wananchi wengine wawili jambo ambalo hawakubaliani nalo.

Kwa upande wake Alloyce Badanga alisema kuwa anamshangaa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa kuwatuma watoza ushuru kwenda kwenye nyumba za wakulima kuwatoza ushuru bila kuwapatia elimu ya aina yoyote.

Alisema kuwa wananchi hawapingi kulipa ushuru lakini ni muhimu wakapata elimu na kuwaelewa utaratibu wa kisheria unavyoelekeza badala ya kuwalazimisha walipe ushuru kwa nguvu.

Akizungumzia suala hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanari Denis Mwila alisema wananchi hao walivunja sheria kwa kujichukulia sheria mkononi na kuanza kuwashambulia watoza ushuru na ndiyo sababu polisi walikwenda kuwakamata.

Hata hivyo alipoulizwa kama watoza ushuru nao walipaswa kwenda kwenye nyumba za wakulima bila hata kupitia kwenye ungozi wa kijiji, Kanari Mwila alikiri kuwa na wao walifanya makosa kwa kutoshirikisha viongozi wa kijiji.



Mkaguzi wa Jeshi la Polisi Kata ya Vwawa, wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe, Fidelia Kasongwa, akitoa elimu ya madhara ya kutokuwa na leseni kwa madereva wa pikipiki maarufu bodaboda wa Kijiwe cha Soko la Vwawa juzi. **PICHA: ISSA MWADANGALA**

# Walalamika kupata umeme mdogo miaka 3

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa eneo la Mavindi Mtaa wa Ilangamoto Kata ya Lyamkena Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe wamelalamika kupata umeme mdogo kwa miaka mitatu mfululizo na hivyo kushindwa kuendesha shughuli zao za kiuchumi.

Wananchi hao wanadai kuwa umeme umekuwa ukikatika kila siku majira ya jioni na kurejea usiku wakiwa wamelala, hali ambayo inawafanya washindwe kuutumia kwa shughuli za uzalishaji ikiwemo uendeshaji wa viwanda.

Wananchi hao walisema licha ya kufikishiwa huduma ya umeme katika eneo lao bado umekuwa hauna msaada kwa sababu wanapata umeme mdogo na hivyo kupata huduma hiyo majira ya usiku.

Hivyo, wameliomba Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) wilaya ya kitanesco Makambako kutatua adha hiyo na kueleza kuwa wapo tayari kuchangia fedha ili kununua transfoma.

Wakizungumza na waandishi wa habari wananchi hao akiwemo Henrick Malekela alisema umeme uliongizwa tangu mwaka 2021 hauna nguvu hali ambayo inasababisha kukosa huduma hiyo majira ya usiku.

Naye Joseph Lungwega alisema kutokana na changamoto hiyo vitu mbalimbali vimekuwa vikiungua ikiwemo luninga na redio.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Ilangamoto, Thomas Kiwale alisema tatizo hilo lipo na tayari amelifikisha kwenye ofisi za Tanesco Makambako.

Diwani wa Kata ya Lyamkena, Salumu Mlumbe alisema licha ya eneo hilo kupata umeme mdogo bado kuna maeneo mengine ya mtaa huo na kata yake kwa ujumla hayajafikwa na huduma hiyo.

## CCM yapiga marufuku ukodishaji mashamba ya shule

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimepiga marufuku mashamba ya shule kukodishwa kwa watu binafsi na badala yake yatumike kwa ajili ya kuzalisha chakula cha wanafunzi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), Ndele Mwaselela alipiga marufuku hiyo juzi alipokuwa anazungumza na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema utaratibu wa wazazi kuchangia chakula cha mchana kwa ajili ya watoto wao ni mzuri lakini unatakiwa kuongezewa nguvu kwa wanafunzi kuzalisha chakula kwenye mashamba mbalimbali yaliyopo kwenye shule hizo.

Alisema shule nyingi za maeneo ya vijijini zina mashamba mengi ambayo zamani yalikuwa yanatumika kuzalisha chakula cha wanafunzi lakini kwa sasa yanakodishwa kwa watu binafsi hali ambayo inasababisha wanafunzi wasijifunze shughuli za kilimo.

## Wanafunzi vyuo vikuu kujengewa uwezo kujiajiri

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI katika vyuo vikuu vitatu nchini watapata fursa ya kujengewa uwezo na maarifa katika kutafuta ajira au kujiajiri baada ya kumaliza masomo yao.

Wanafunzi hao watafaidika kupitia mradi wa 'Generation Empower' ambapo watapewa elimu kupitia semina mbalimbali pamoja na kujifunza kupitia mtandao wa intaneti.

Akizungumza jana kwenye hafla ya utiaji saini makubaliano ya ushirikiano kati ya taasisi ya Empower na Tigo, Mkurugenzi mwenza wa taasisi hiyo, Miranda Naiman, alisema mradi huo utaendeshwa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Dodoma (UDOM). Chuo cha Mtakatifu Agustino (SAUT) na Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM).

Alisema kupitia mradi huo wanafunzi watapata fursa kupata elimu juu ya masuala ya ajira pamoja na kujengewa uwezo wa kuweza kujiajiri baada ya kumaliza masomo.



# Serikali yachukua hatua kukabiliana uhaba wa dola

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imechukua hatua za kukabiliana na uhaba wa dola mojawapo ikiwa ni kuuza fedha za kigeni kwenye Soko la Jumla la Fedha za Kigeni (IFEM) na kuendelea kufanya malipo mbalimbali kwa niaba ya serikali.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Juma Makungu alitoa taarifa hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Mohammed Ali Suleiman.

Mwakilishi huyo alitaka kujua serikali inachukua hatua gani za haraka kushughulikia uhaba wa dola na kuhakikisha utulivu wa masoko ya fedha.

Akijibu swali hilo, Juma alisema BoT ilikuwa tayari imeshauza Dola za Marekani milioni 555 kupitia IFEM ili kupunguza upungufu wa fedha za kigeni nchini.

Alisema serikali kupitia BoT imeendelea kutekeleza sera mpya ya ushiriki kwenye soko la jumla la fedha za kigeni ambapo sera hiyo ilianza kutumika Januari 2024.

Makungu alisema katika mpango huo, benki 18 zimenufaika na tathmini ya miamala ya fedha za kigeni inayoonyesha kuwa sekta zilizonufaika ni pamoja na mafuta (20.35%), biashara (24.40%) na viwanda (6.16%).

Aidha, alisema serikali imekua na mikakati ya kuimarisha upatikanaji wa dola na kuzuia athari za uhaba huo kwa biashara na uchumi wa Zanzibar ikiwemo serikali kupitia BoT imetoa kanuni mpya za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni za mwaka 2023 ili kurahisisha utoaji wa leseni kwa maduka hayo.

Alisema mabadiliko hayo yameongeza idadi ya maduka ya kubadilisha fedha za kigeni nchini, kwamba hadi Aprili 2024, BoT imetoa leseni 21 zenye matawi 100, ikilinganishwa na maduka 12 yenye matawi 81 yaliyokuwepo Desemba mwaka 2023.

Hata hivyo, alisema serikali kupitia BoT imetoa sera ya ushiriki kwenye soko la jumla la fedha za kigeni iliyoanza kufanya kazi Januari 2024.

Alisema mipango ya muda mrefu itakayoweza kupunguza uhaba wa dola nchini ni pamoja na kuimarisha uzalishaji wa ndani ili kupunguza kuingiza bidhaa nyingi nchini.

Mpango mwingine ni kusimamia utaratibu wa uendeshaji wa masoko ya fedha za kigeni ya jumla na rejareja ili kurahisisha biashara, hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kwa njia rasmi.

"Kwa hiyo serikali imefanya mambo mbalimbali ikiwemo kuendelea kuongeza akiba ya fedha ya kigeni na hivyo kuongeza uwezo wa kuuza Dola za Marekani katika soko la fedha za kigeni nchini," alisema.

Alisema hadi kufikia Aprili 2024, BoT imefanya miamala ya kubadilisha fedha za kigeni na benki za biashara yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 147.

# Kitengo cha usuluhishi kuanzishwa mahakama za kadhi

**Na Mwandishi Wetu**

IDARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inatarajia kuanzisha kitengo cha usuluhishi katika mahakama za kadhi ili kupunguza mlundikano wa kesi zinazohusiana na wanawake na watoto.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Idara hiyo, Siti Abasi Ali wakati akizungumza na makadhi wa mikoa ya Unguja, kikao kilichofanyika Wilaya ya Mjini.

Alisema lengo la kuanzisha kitengo hicho ni kuweka mikakati bora na imara ya kutatua kesi hizo kwa uhakika na kuondosha manung'uniko kwa jamii.

Alisema makadhi hao wanapokea kesi nyingi na wakati mwingine wanalazimika kutoa uamuzi kwa haraka kutokana na wengi wake jambo ambalo linachangia ongezeko la talaka na kusababisha utelekezaji wa wanawake na watoto.

Aidha, alisema vituo hivyo vitapunguza kesi katika jamii ikiwemo mirathi, migogoro ya ndoa na huduma za watoto.

Mratibu wa mapambano ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto kutoka idara hiyo, Omar Haji Omar, alisema utafiti unaonyesha kuwa idadi kubwa ya talaka inasababisha utelekezaji wa watoto katika jamii.

Hivyo, aliwataka vijana kuacha kufunga ndoa kwa kufuata mkumbo na mihemko na badala yake wapate elimu kabla ya kufunga ndoa na kuifanyia kazi.

Alisema talaka ni chanzo cha watoto kutelekezwa na kuharibika na kuwataka wanandoa kuwaza watoto wao kabla ya kuachana ili kuwaondolea usumbufu unaojitokeza baadaye.

Baadhi ya makadhi hao, akiwemo Kadhi wa Wilaya ya Mjini, Sheikh Ali Juma Machano na Kadhi wa Wilaya ya Magharibi B, Sheikh Abubakar Ali mohammed walisema juhudi za kutoa elimu katika jamii bado zinahitajika ili kuondosha utoaji wa talaka kiholela.

Aidha, walishauri idara hiyo kuwa na mpango wa kuhakikisha masuala ya usuluhishi wa migogoro ya ndoa inaanzia katika madawati ya jinsia katika ngazi ya shehia pamoja na kuwepo mikakati madhubuti ya kuzinusuru ndoa kwa maslahi ya kizazi cha sasa na kijacho.

**Talaka ni chanzo cha watoto kutelekezwa na kuharibika na kuwataka wanandoa kuwaza watoto wao kabla ya kuachana ili kuwaondolea usumbufu unaojitokeza baadaye.**



Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Salha Muhammed Mwinjuma, akizungumza wakati wa kipindi cha maswali na majibu katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SUZA yaanzisha kigoda cha Hayati Abeid Amani Karume

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHUO Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kimeandaa kigoda cha taaluma cha Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, lengo likiwa ni kuhifadhi, kuenzi na kuendeleza mawazo na fikra za kiongozi huyo katika kuleta ukombozi na maendeleo Tanzania, Afrika na duania.

Akizungumza na waandishi wa habari, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Muhamed Makame Haji alisema kigoda hicho kitahusika kufanya utafiti na mijadala mbalimbali ya kitaaluma ili kukabiliana na changamoto katika nyanja za kiuchmi, kijamii, kiutamaduni, kisayansi na kifikra.

Alisema pia kuifanya SUZA kuendeleza adhma yake ya kuwa kichocheo cha mabadiliko ya jamii.

Alisema katika kufanikisha lengo hilo kigoda hicho ni kuhifadhi kuibua na kueneza mawazo na fikra za Hayati Abeid Amani Karume kupitia utafiti, mijadala, makongamano, mikutano na machapisho.

Aidha, alisema pia kigoda kitakuza uwezo wa vijana wasomi wanaochipukia kwa kuwashirikisha katika utafiti, makongamano, mikutano, mijadala, kuwasaidia kupata fedha za mikopo na masomo ya utafiti.

Pia alisema uzinduzi wa kigoda hicho utafanyika Juni 15 mwaka huu chuoni hapo ambao utaenda sambamba na maonesho ya utafiti na huduma kwa jamii, mgeni rasmi anatarajia kuwa Rais wa Zanzibar, Dk .Hussein Ali Mwinyi.

Alisema wageni mbalimbali mashuhuri wanatarajiwa kushiriki katika uzinduzi huo wakiwemo marais wastaafu akiwemo Dk. Jakaya Kikwete, Dk. Ali Mohamed Shein, Amani Abeid Karume na mabalozi wa nchi mbalimbali pamoja na viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAINES JAKINA MWAKIBINGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.5025/0014 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KEIFO SECONDARY SCHOOL mwaka 2021. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/PWA/BAG/10116/2024**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**MATRIMONIAL/CAUSE NO. 5013 OF 2024**
**VERONICA FREDDRICK KAIGI ............APPELANT**
**VERSUS**
**STEVEN HAMIS MILAMBO.........RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF MENTION/HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention/Hearing on 25 day of JUNE 2024 at 9:00 am Before HON SWAI SRM

You are required to appear in this court without failure and you must produce to that day all the documents upon which you intended to reply in support of your case.

GIVEN under my hand and SEAL of the court this 21 day of MAY 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEORGE AMANI PATRICK** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4884- 0036 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KIZUMBA SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/UBU/113868/2024**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO. 13622/2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**NELSON ISSA NDELWA**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by**
**BETISEBA LOTI SANGA..................PETITIONER**

**(GENERAL CITATION (RULE 75)**

**ALL PERSONS** claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of July, 2024

**Dated at Kyela this 12th day of June,2024**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 13617/2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**SALVATORY PAULO MONELA**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by**
**CATHERINE DEVES CHILIMBA...............PETITIONER**
**(GENERAL CITATION (RULE 75)**

ALL PERSONS claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of July, 2024

Dated at Kyela this 12th day of June,2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 11903 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**ANASTAZIA ITIRIGO TEMBO**

**By 1: MARWA ABDUL TEMBO**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 26TH day of JUNE.2024

Dated at MOROGORO this 07TH day of JUNE.2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GUTA

**GRACE CHRISTIAN OLOMI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya guta yenye USAJILI NAMBA: MC 490 DAY, CHASSIS NAMBA: LATZDMZY4M5931589 na ENGINE NAMBA: M5160735. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/DOD/DOD/21424/2024**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 11903 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**ANASTAZIA ITIRIGO TEMBO**

**By 1: MARWA ABDUL TEMBO**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 26TH day of JUNE.2024

Dated at MOROGORO this 07TH day of JUNE.2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,

WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## MIEZI MITATU AJALI ZA ANGA:

# Zaacha simanzi kwa mataifa matatu, wamo Rais, Makamu wa Rais




**Christina Mwakangale na Mitandao**

KWA miezi mitatu mfululizo ajali za anga zimetikisa dunia, huku zikisababisha vifo kwa abiria waliomo ndani, wakiwamo viongozi wakuu katika nchi tatu.

Ajali hizo ni pamoja na ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini Kenya Francis Ogolla, Aprili mwaka huu; Rais wa Iran, Ebrahim Raisi, Mei mwaka huu; Makamu wa Malawi Saulos Chilima, iliyotokea wiki hii.

Mbali na ajali hizo kusababisha vifo vya viongozi hao, zimesababisha idadi ya watu 27 kupoteza maisha wakiwamo maofisa wakuu wa serikali.

Kwa mujibu wataalam wa usafirishaji, usafiri wa anga ni miongoni mwa usafiri salama zaidi, kati ya aina tatu ambao ni anga; ardhini (reli na barabara); maji.

Narscent Meena, rubani binafsi amezungumza na Nipashe, jana, kuhusu usalama wa usafiri wa anga na tahadhari za kuchukua kabla na wakati wa safari angani.

"Kwanza kila ndege au helikopta kabla haijaruka tunaangalia ndege ya abiria itabeba watu wangapi, ili ndege iwe na uwiano na inakwenda wapi itaruka futi ngani, mafuta kiasi gani itabeba.

"Pia, mhandisi anaikagua, anajidhihirisha kabla ndege haijaondoka iko sawa, anasaini na kuikabidhi kwa rubani. Kuna watu wa 'road control' wanahaikisha uwiano inaporuka na kutua viko sawa," anasema.

Anasema kwamba pamoja na ajali za ndege za viongozi kufululiza, bado usafiri wa anga ni salama, akisema mabadiliko ya hali ya hewa ghafla pamoja kupoteza mawasiliano, huweza kumuathiri rubani.

"Tatizo la kiafya huweza kumuathiri rubani ghafla na pia rubani kuiamini ndege yake kwamba inaweza kufanya kazi vizuri, ila tahadhari huchukuliwa bila kujali imebeba viongozi au la."

**JUNI MWAKA HUU**

Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera, ametangaza siku 21 za maombolezo kitaifa hadi Julai Mosi, mwaka huu, kufuatia kifo cha Makamu wa Rais, Dk. Saulos Chilima, kilichotokana na ajali ya ndege, Jumatatu, wiki hii.

Kwenye ajali hiyo, walikuwamo pia watu tisa nao wakifariki dunia. Ajali ilitokea katika hifadhi ya misitu wa Chikangawa, Juni 10, mwaka huu.

Ndege hiyo ilikuwa unaelekea kutua katika uwanja wa Kimataifa Mzuzu, uliopo kilomita 380 kutoka Kaskazini mwa mji Mkuu Lilongwe.

Chilima, na maofisa wengine alikuwa akisafiri kuhudhuria mazishi ya aliyekuwa Waziri wa serikali hiyo, Ralph Kasambara.

Mke wa rais wa zamani Bakili Muluzi, Shanil Dzimbiri ni miongoni mwa abiria waliokuwa kwenye ndege hiyo, kwa mujibu wa taarifa ya rais Chakwera.

Ndege aina ya Dornier 228 ilitangazwa kupotea kwenye rada ilipofikia eneo la hifadhi ya misitu Chikangawa na June 11, mwaka huu, ikathibitishwa imepata ajali.

Chilima, alikuwa mwanasiasa maarufu katika siasa za Malawi, na kabla ya kujiunga na siasa alichangia kujua kwa kampuni ya Airtel nchini humo na kukuza mapato.

Kisiasa, amehudumu katika kiti hicho tangu mwaka 2014 akipambana na rushwa na kukumbana na changamoto kadhaa.

Mazishi ya kitaifa yanaangazia mchango wake katika nchi.

Chilima alikuwa amerejea tu kutoka katika ziara ya kikazi nchini Korea Kusini, kwenye kongamano la Korea Afrika Summit, mjini Seoul, siku ya Jumapili, mwishoni mwa wiki.

Chilima, ameacha mke Mary mmna watoto wawili.

**APRIL MWAKA HUU**

April, mwaka huu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini Kenya, Francis Ogolla alifariki kwa ajali ya helikopta.

Rais wa Kenya, William Ruto alitangaza kifo cha Ogolla pamoja na maofisa wengine tisa wa jeshi, huku wawili wakinusurika.

Ogolla alifariki baada ya helikopta aliyokuwa akisafiria pamoja na maofisa wengine kuanguka eneo la Kaben, Marakwet Mashariki.

Ogolla alichukua nafasi ya kuongoza jeshi tangu April 28, mwaka jana.

Mashuhuda walisema kuwa ilishika moto wakati wa kuanguka. Eneo hilo lilizingirwa mara baada ya ajali hiyo.

Maofisa hao walikuwa wakichunguza eneo hilo kabla ya kutumwa kwa wanajeshi zaidi kukabiliana na wezi wa mifugo katika eneo hilo.

Helikopta hiyo ya jeshi la Anga la Kenya aina ya Huey, ilikuwa imetoka katika shule moja ya msingi ya eneo hilo hadi ilipoanguka na kuwaka moto.

Ogolla, aliteuliwa kuwa Mkuu mpya wa Majeshi ya Ulinzi katika mabadiliko katika jeshi, akichukua hatamu kutoka kwa mtangulizi wake Jenerali Robert Kibochi.

Kibochi alimkabidhi Ogolla kama Mkuu wa majeshi, baada ya kufikisha umri wa kustaafu.

**MEI MWAKA HUU**

Mei, mwaka huu, Rais wa Iran, Ebrahim Raisi, pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje, Hossein Amir-Abdollahian na wengine saba, walithibitishwa kufariki dunia katika ajali ya helikopta iliyotokea kaskazini-magharibi mwa Iran, kwa mujibu wa televisheni ya taifa.

Shirika la habari la serikali (IRNAA), lilisema kwamba ndani ya ndege hiyo pia alikuwamo Ayatollah Mohammad Ali Al-e Hashem, imamu wa Swala ya Ijumaa katika mji wa Tabriz, na Jenerali Malek Rahmati, gavana wa jimbo la Iran la Azabajani Mashariki.

Kamanda wa Kitengo cha Ulinzi wa Rais, Sardar Seyed Mehdi Mousavi, pia aliuawa, pamoja na walinzi kadhaa na wafanyakazi wa helikopta ambao bado hawajatajwa.

HABARI MICHEZO

# Zimamoto yaichapa Mephis kikapu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAAFANDE wa Zimamoto wameifunga Mephis 96-67 katika mechi ya Ligi ya Kikapu Kanda ya Unguja iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau Kisiwani juzi usiku.

Katika mchezo huo, Zimamoto ilianza kuwazima Mephis tangu 'kota' ya kwanza mchezo huo kwa kufunga vikapu 11-19 na hadi wanakwenda mapumziko, Maafande hao walikuwa mbele kwa vikapu 50-23.

Zimamoto iliendelea na mkakati wake wa kuhakikisha ulifanikiwa katika kota hiyo kwa kupachika vikapu 72 -43, hadi kota ya mwisho zimamoto waliendelea kuwa wababe.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena leo kwa Millenium kuwakaribisha Miembeni Pacers.

„Ligi imekuwa na msisimko mkubwa kwa sababu ya viwango vinavyoonyeshwa na wachezaji wa timu zote, tumeshuhudia mechi zenye ushindani wakati wote, tunaamini tutapata vikosi na wawakilishi imara kwa ajili ya timu za taifa," Said Ameir, mdau wa mchezo huo, alisema.

## Karate wajipanga na Kanda ya Tano

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Karate Tanzania (TSKF) limeanza kusaka wachezaji watakaounda timu ya taifa kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kanda ya Tano yatakayofanyika jijini Nairobi, Kenya mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa TSKF, Sensei Mgeni, alisema wameunda kamati maalum inayoangalia wachezaji wenye viwango vinavyostahili kuwapo katika kikosi hicho ili kuwaweka kambini kuwanoa.

„Kwa mujibu wa kalenda yetu kuna mashindano ya taifa yatakayofanyika Juni na Desemba, mwaka huu, tutayatumia kuchagua timu ya taifa, tutafunga zoezi la kuteua wachezaji Desemba na kuanza programu za mazoezi mapema", alisema Mgeni.

Aliongeza viwango vya wachezaji kwa sasa vimepanda kutokana na ushiriki wa timu za Zanzibar tofauti na mwamko mdogo uliokuwapo katika miaka ya nyuma.

Wakati huo huo, Island Warrior kutoka Zanzibar imeibuka mshindi wa mashindano ya Kumite ikifuatiwa na Serengeti wakati Kibaha Shotokan imemaliza katika nafasi

# YANGA, SIMBA ZAUNGANA KUIBOMOA SINGIDA BS FC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI uongozi wa Singida Black Stars ukipania kutengeneza kikosi chake kwa ajili ya msimu mpya, vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga zimebisha hodi katika timu hiyo kwa lengo la kuwasajili nyota wa timu hiyo ambayo zamani ilijulikana kwa jina la Ihefu, imefahamika.

Singida Black Stars iko katika hatua za mwisho za kumsajili winga raia wa Niger, Victorien Adebayor.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo inasema huenda wakawapoteza wachezaji wao wawili nyota, winga, Emmanuel Bola Lobota, anayetakiwa na Yanga huku Simba ikitaka kumng'oa beki wa kati, raia wa Nigeria, Benjamin Tanimu.

Chanzo chetu kinasema Yanga imekamilisha taratibu za kumsajili winga huyo anayecheza upande wa kushoto, lakini anaweza pia kucheza kulia wakati Simba iko katika hatua za mwisho kumnasa Tanimu.

„Tunafanya usajili mkubwa wa wachezaji wa ndani na nje, tunataka kutengeneza timu ya ushindani, lakini katika usajili kuna mambo mengi, wakati sisi tunasajili, wapo wachezaji watakaoondoka.

Simba nao wanamkata huyu beki wetu Tanimu, wameonekana kuvutiwa naye, unajua wana tatizo hilo kwani wanataka awe mbadala wa Henock Inonga, anayetajwa huenda akatua FAR Rabat ya Morocco, nao wakikamilisha sawa, sisi hatuna tatizo, tutaleta wengine," alisema mtoa habari huyo.

Mbali na Adebayor, mchezaji ambaye alitakiwa na Simba misimu mwili mfululizo iliyopita, Singida Black Stars iko mbioni kupata saini za wachezaji, Hervy Ossete, kiungo mkabaji Mkongomani, beki wa kushoto, Ibrahim Imoro kutoka Al Hilal ya Sudan na golikipa, Mohamed Kamara wa Horoya ya Guinea.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema siku si nyingi wataanza kutaja mchezaji mmoja mmoja atakayekuwa amesajiliwa na timu yao.

„Tuwaache kwanza wachezaji wapumzike, mashabiki nao nawataka wapumzishe akili zao, kila kitu kitakuwa wazi muda ukifika, tutaanza kuweka mambo hadharani, wanaotoka, wanaoingia, ratiba ya 'preseason' na Tamasha la Simba Day," alisema Ahmed.

Kwa upande wa Yanga, Ali Kamwe, alisema wao kwa asilimia kubwa wameshamaliza kusajili, kilichobakia ni kuwatangaza tu.

„Tumeshafanya usajili, kama Rais wa klabu yetu Injinia Hersi alivyosema tutasajili wachezaji wa viwango vya juu na kweli, vyuma kweli kweli, muda wa kuwatangaza ukifika tutafanya hivyo," alisema.

**SOKA WANAWAKE**

**Mshambuliaji wa Mpaju Queens ya Mbeya (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Gets Program katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza kwa Wanawake (WFDL) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Fountain Gate jijini Dodoma jana. Gets Program ilishinda mabao 2-0. PICHA: TFF**



# JKT TZ, JKT QUEENS KUBORESHWA

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa JKT Tanzania umesema wanasubiri kumalizika kwa msimu wa Ligi Kuu ya Wanawake Nchini (TWPL) ili waanze mchakato wa usajili wa wachezaji wa timu zao mbili kwa pamoja.

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) inamiliki timu ya JKT Tanzania inayoshiriki Ligi Kuu Bara na JKT Queens, inayocheza Ligi ya Wanawake.

Msemaji wa taasisi hiyo, Masau Bwire, alisema wanatarajia kuzifanyia kazi kwa pamoja taarifa ya Malale Hamsini wa JKT Tanzania na kutoka kwa Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma.

„Kwa sasa tunasubiri Ligi ya Wanawake imalizike ili tuanze kufanya usajili kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao, tutajipanga na kujiimarisha, tutaangalia mapungufu yetu na kujiimarisha vyema,"alisema Bwire.

Aliongeza malengo yao ni kujiimarisha ili kilichowakuta msimu huu cha kupambana kujinusuru na janga la kushuka daraja kisijirudie kwa kuanza maandalizi yote muhimu mapema.

Winga tegemeo wa JKT Tanzania, Shiza Kichuya, ameutaka uongozi wa timu yao kumsajili, Bernard Morrison, katika kikosi chao.

Hata hivyo bado Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), halijafungua rasmi dirisha la usajili.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**LUIZ AKARIBIA JUVENTUS**
JUVENTUS wamepiga hatua katika juhudi yao ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Douglas Luiz, mwenye umri wa miaka 26, kutoka Aston Villa. ***(Sky Sports)***

**DURAN KUTUA CHELSEA**
CHELSEA imefufua nia yao ya kumnunua mshambuliaji wa Aston Villa na Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Duran, mwenye umri wa miaka 20. ***(Telegraph)***

**COLWILL SOKONI EPL**
MLINZI wa Chelsea na England, Levi Colwill, mwenye umri wa miaka 21, bado ananyatiwa na Bayern Munich ambao pia wanataka kumnunua beki wa Ujerumani na Bayer Leverkusen, Jonathan Tah, mwenye miaka 28. ***(Sky Germany)***

**UNITED, ARSENAL VITANI**
KLABU ya Manchester United inajiandaa kuchuana na Arsenal katika harakati zao za kumnunua mshambuliaji wa Bologna, ambaye ni raia wa Uholanzi, Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 23, akiwa na kipengele cha kuachiliwa cha pauni milioni 34. ***(Metro)***

**OBI-MARTIN ATAJWA BAYERN**
ARSENAL inakabiliwa na changamoto ya kumbakisha mashambuliaji wa chini ya miaka 17 wa Denmark, Chido Obi-Martin, mwenye miaka 16, ambaye anasakwa na Bayern Munich. ***(Metro)***

**UNITED KUNASA MASTRAIKA**
KLABU ya Manchester United imeandaa orodha fupi ya washambuliaji huku straika wa Brentford na England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 28, na mshambuliaji wa Lille na Canada, Jonathan David (24), wakizingatiwa sana. ***(ESPN)***

**JOHNSON MKATABA BORA**
KLABU ya West Ham imempa beki wa Timu ya Taifa ya England, Ben Johnson, mwenye umri wa miaka 24, mkataba ulioboreshwa wa miaka mitano. ***(Athletic)***

**MVUMPA ANUKIA FULHAM**
FULHAM inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumnunua, Silas Katompa Mvumpa, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Stuttgart, huku fowadi huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), akiwa na thamani ya pauni milioni 15. ***(HITC)***

**TIERNEY ASHUSHWA THAMANI**
ARSENAL iko tayari kumuuza mlinzi wa Scotland, Kieran Tierney, kwa hasara msimu huu, na ofa ya pauni milioni 15 itatosha kumpata mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

**GROSS, BRIGHTON KUTETA**
KIUNGO wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross, mwenye umri wa miaka 32, anajadiliana na Brighton kuhusu kuongeza mkataba wake. ***(Athletic)***

**NEVETT AGEUKA LULU**
KLABU za Crystal Palace, Ipswich na Southampton zinamwania beki wa Rochdale, George Nevett, mwenye umri wa miaka 18, kutoka Wales. ***(HITC)***



# SOUTHGATE: NITAONDOKA NISIPOSHINDA EURO 2024

●●●Kocha huyo wa England asema hii ni nafasi yake ya mwisho...

**LONDON,** ENGLAND

GARETH Southgate amesema kuna uwezekano akaacha nafasi yake kama Kocha wa Timu ya Taifa ya England endapo timu hiyo itashindwa kushinda Kombe la Euro 2024.

Mkataba wake unamalizika Desemba, ingawa vyanzo viliiambia ESPN, Chama cha Soka England, kingependa aendelee na jukumu hilo.

Southgate mwenye umri wa miaka 53, ambaye alichukua jukumu hilo mwaka 2016, amesimamia mabadiliko makubwa na kuiongoza England kufika nusu fainali ya Kombe la Dunia la 2018 na kupoteza fainali ya Euro 2020 kwa penalti dhidi ya Italia kwenye Uwanja wa Wembley.

England ilitolewa Kombe la Dunia 2022 katika hatua ya robo fainali na Ufaransa.

Rekodi hiyo ya jumla ya mashindano, pamoja na kuibuka kwa wachezaji wachanga wa kusisimua akiwamo, Jude Bellingham, Cole Palmer, Anthony Gordon na Kobbie Mainoo, imeongeza matarajio kwa Euro ya mwaka huu.

Southgate nusura ajiuzulu baada ya Kombe la Dunia 2022.

Aliliambia gazeti la Ujerumani la Bild: „Ikiwa hatutashinda Euro, labda sitakuwa hapa tena. Basi inaweza kuwa nafasi ya mwisho.

„Nadhani takriban nusu ya makocha wa kitaifa wanaondoka baada ya mashindano, hiyo ndiyo hali ya soka ya kimataifa. Nimekuwa hapa kwa takriban miaka nane sasa na tumekaribia.

"Kwa hiyo najua huwezi kuendelea kusimama mbele ya umma na kusema: 'Tafadhali fanya zaidi kidogo,' kwa sababu wakati fulani watu watapoteza imani katika ujumbe wako.

„Ikiwa tunataka kuwa timu kubwa na ninataka kuwa kocha wa juu, basi lazima ufanye kazi katika wakati muhimu."

Southgate aliiambia ESPN mwezi uliopita Kombe la Dunia la 2026 nchini Marekani, Canada na Mexico litakuwa „mashindano ya kustaajabisha" lakini akasisitiza hajaamua kama ataendelea.

# LEWANDOWSKI AIPA PIGO POLAND

**BERLIN,** UJERUMANI

TIMU ya Taifa ya Poland imethibitisha, Robert Lewandowski, ataukosa mchezo wao wa ufunguzi katika michuano ya EURO 2024.

Poland watavaana na Uholanzi katika mchezo wao wa kwanza wa Kundi D utakaochezwa Jumapili.

Lakini itawabidi kuucheza mchezo huo mgumu bila ya straika huyo anayeichezea Barcelona ambaye amepata majeraha ya msuli wa paja.

Lewandowski alishindwa kumaliza mchezo wa kirafiki dhidi ya Uturuki uliochezwa juzi na taarifa nyingine zinasema huenda akakosa michuano yote ya Euro.

Lakini, Shirikisho la Soka la Poland limetoa maelezo, licha ya kuwa fowadi huyo kuukosa mchezo wa ufunguzi, kitengo chao cha madaktari kitafanya kila liwezekenalo kumrudisha nyota huyo uwanjani katika mchezo wao wa pili dhidi ya Austria.




# Ten Hag sasa uhakika kubaki Man United



**MANCHESTER,** ENGLAND

MANCHESTER United wameamua, Erik ten Hag, atabaki kama kocha wao, chanzo kimeithibitishia ESPN.

Mustakabali wa Mholanzi huyo umekuwa mashakani kufuatia kampeni mbaya katika Ligi Kuu England msimu uliomalizika.

Lakini msimu ulimalizika kwa hali ya juu baada ya United kushinda Kombe la FA dhidi ya wapinzani wao, Manchester City na kufuatia ukaguzi wa mwisho wa msimu uliofanywa na wamiliki wenza wapya, INEOS na kuongozwa na Sir Dave Brailsford, uamuzi umechukuliwa ili kumbakisha Ten Hag.

Chanzo kiliiambia ESPN "hitimisho wazi" la ukaguzi lililofikiwa Ten Hag abaki kama kocha.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Ten Hag na United wanatazamiwa kujadili kuongezwa kwa mkataba wake, ambao ulipaswa kumalizika mwakani, baada ya "majadiliano yenye kujenga" kuhusu matokeo ya ukaguzi huo.

Ten Hag mwenye umri wa miaka 54, alifurahia msimu wa kwanza pale Old Trafford, akimaliza wa tatu kwenye Ligi Kuu na kushinda Kombe la Carabao.

Lakini msimu wake wa pili aliokolewa tu kwa kunyanyua Kombe la FA baada ya kampeni mbaya kwenye ligi na Ulaya.

United iliishia nafasi ya nane katika jedwali na kuweka rekodi ya kumaliza chini kabisa katika Ligi Kuu England.

Pia ilimaliza mkiani mwa kundi lao kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Iliifanya United kutafuta mbadala wa Ten Hag akiwamo Thomas Tuchel, Mauricio Pochettino, Roberto De Zerbi, Thomas Frank, Kieran McKenna na Graham Potter.

Pia kumekuwa na nia ya kumtaka Kocha wa England, Gareth Southgate.

Ten Hag amekuwa akisisitiza mara kwa mara majeraha yaliyosababisha matokeo mabaya.

Baada ya kupata uthibitisho ataendelea na kazi yake, anatarajiwa kurejea Carrington kwa ajili ya kuanza kwa mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya mapema Julai.

# Diaz: Nina furaha Liverpool

**LIVERPOOL,** ENGLAND

LUIS Diaz amesisitiza "nina furaha na sina wasiwasi" huku kukiwa na uvumi unaoendelea kumhusisha na kuondoka Liverpool.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 aliichezea Liverpool mechi 37 za Ligi Kuu England msimu uliopita, na kusajili mabao nane huku Wekundu hao wakimaliza nafasi ya tatu nyuma ya Manchester City na Arsenal.

Diaz amekuwa akihusishwa mara kwa mara anataka kuondoka Liverpool, ambayo alijiunga nayo kutoka Porto miaka mitatu iliyopita, huku Paris Saint-Germain na Barcelona zikitajwa kumwania.

Ripoti kutoka Hispania zimedokeza, Diaz ndiye anayelengwa zaidi na Barcelona, licha ya matatizo yao ya kifedha yanayoendelea, lakini maoni ya hivi punde ya winga huyo, kufuatia kipigo cha mabao 5-1 cha Colombia dhidi ya Marekani - yanaonyesha hana nia ya kuondoka Anfield.

"Nina furaha sana pale Liverpool, ni timu kubwa na nimekuwa nikitamani kucheza huko, kwa hiyo nina furaha na utulivu," alisema Diaz akiiambia Gol Caracol.

"Sifikirii juu ya kitu kingine chochote, ninafikiria kuhusu timu ya taifa ya Colombia, ambayo ndio tulipo."

Tetesi za kutaka PSG kumtaka Diaz zimeongezeka baada ya uhamisho wa Kylian Mbappe kwenda Real Madrid kuthibitishwa, lakini wababe hao wa Ligue 1 watalazimika kulipa gharama kubwa ili kuwashawishi Liverpool kumuuza.

Diaz amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake wa sasa.

Wakati huo huo, Barcelona huenda ikahitaji kuuza wachezaji ili kufadhili biashara yao ya uhamisho wa majira ya kiangazi, huku kocha wa zamani wa Bayern Munich, Hansi Flick, akipewa jukumu la kusawazisha meli baada ya Xavi kuondoka.

Miamba hao wa Katalunya wako tayari kuachana na Raphinha, ripoti zinaonyesha, na dili la kubadilishana linalomhusisha kiungo wa kati wa Manchester United, Kobbie Mainoo, limefutika.

HABARI MICHEZO

# STARS YAFUNGUKA ILIIMALIZA CHIPOLOPOLO IKIWA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Kati wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Bakari Mwamnyeto, amesema waliimaliza mechi dhidi ya Zambia (Chipolopolo), wakiwa Tanzania na ugenini Ndola walikwenda kukamilisha kile walichoelekezwa na benchi la ufundi.

Taifa Stars iliifunga Chipolopolo bao 1-0 katika mechi ya Kundi E ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa mjini Ndola, juzi usiku.

„Kila kitu kilifanyika Dar es Salaam, tulikuja hapa kukamilisha mchezo. Tulishawasoma, tangu tuko Dar es Salaam, walimu wetu walifanya kazi hiyo, wakatuambia mazuri yao yako wapi na mabaya yao, tumeweza kutumia udhaifu wao, tukapata bao mapema, tumewakabili kwa sababu tayari tulishawajua wachezaji wao hatari, na kila mmoja ubora wake upo sehemu gani, tukawabana hadi mwisho.

Niwashukuru wachezaji wenzangu, tumepambana kwa kiasi kikubwa, tumejitolea kwa moyo, jasho na damu," Mwamnyeto alifichua siri hiyo.

Kocha Mkuu, Hemed Morocco, alikiri mechi ilikuwa ngumu, lakini walijipanga tangu wakiwa nchini na kujua wanakwenda kucheza na timu ya aina gani.

„Mechi ilikuwa ngumu, tulijua kabisa tunacheza na timu ya taifa ya Zambia, ni timu ambayo ilipoteza mchezo uliopita dhidi ya Morocco, hawako katika nafasi nzuri, wanacheza nyumbani mbele ya wapenzi wao, lakini tulijipanga kuhakikisha tunaizima hiyo presha yao.

Nashukuru wachezaji wangu kwa sababu haikuwa rahisi, tumeweza kupambana dakika zote 90, mfumo tuliokuja nao umeweza kufanya kazi, niseme tu kuwa hii imeisha tuangalie mbele zaidi," Morocco alisema.

Katika siku za hivi karibuni Taifa Stars imekuwa ikifanya vyema zaidi wanapokuwa ugenini, huku baadhi ya wachezaji wakisema presha ya ugenini huwa ndogo ukilinganisha na wanapokuwa nyumbani.



Kikosi cha mabingwa wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), Simba Queens, ambao kesho watakabidhiwa kombe la ubingwa wa ligi hiyo baada ya kumaliza mechi ya mwisho dhidi ya Geita Gold itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# Waziri Jr : Nimeanza vizuri Stars

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Waziri Junior, amesema amefurahi kuanza vizuri katika mchezo wake wa kwanza wa mashindano na timu hiyo, ambapo iliibuka na ushindi wa bao 1-0.

Waziri Jr alifunga bao pekee katika mechi hiyo na kuifanya Stars ifikishe pointi sita na kupaa hadi nafasi ya pili kwenye Kundi E katika mbio za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

Nyota huyo wa KMC alifunga bao dakika ya tano baada ya kupokea pasi ‚ya upendo' kutoka kwa Mudathir Yahya, aliyempokonya mpira kiungo wa Zambia kabla ya kutoa pasi kwa mfungaji.

Baada ya mechi hiyo kumalizikia, Waziri Jr alisema anaamini mwanzo huo mzuri ni ishara njema kwake katika kuitumikia taifa.

„Nafurahi sana kwa timu yetu kupata ushindi huu muhimu, kwangu ni mwanzo mzuri kwa sababu huu ndio mchezo wangu wa kwanza wa kimashindano nikiwa katika kikosi cha Taifa Stars, nashukuru kwa mwanzo huu mzuri," alisema Waziri.

Aliongeza ushindi huo wa ugenini utawaongezea morali kuelekea michezo mingine iliyobakia kabla ya kujua hatima yao.

Morocco yenye pointi sita sawa na Taifa Stars ndio vinara wa Kundi E wakati Niger wanashika nafasi ya tatu kwa kubaki na pointi zao tatu sawa na Zambia wakati DRC ni ya tano na Eritrea inaburuza mkia katika kundi hilo.

## Sinema yakolea Simba SC

INATOKA UK. 24

ma na wapenzi, nitashirikiana na viongozi wenzangu ili kukamilisha mchakato wa mabadiliko ili Wana- Simba wapate hisa zao stahiki na kuwa wamiliki kamili wa klabu, hili ni muhimu katika ukuaji wa klabu, tano ni miundombinu ya klabu iliyopo Bunju haikidhi haja, hivyo ni lazima tulifanyie uwekezaji ulio bora kufanana na hadhi ya Simba.

Mkakati wa sita, Simba inahitaji kuwa na mchakato wa kuibua vipaji, tutalifanyia kazi zaidi," aliahidi bilionea huyo na hapo hapo alitangaza kumteua Try Again kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

Pia amewataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuimarisha umoja wao kwa sababu hakuna muda tena wa kulalamika, kupiga kelele na kupakana matope, bali wanatakiwa kuijenga Simba mpya.

„Nimemwomba Salim (Try Again), kubaki kwenye bodi kwa niaba ya mwekezaji na amekubali, na hivi karibuni nitateua wajumbe wengine ili bodi iwe kamili kuanza kazi. Narejea nikiwa na nguvu na ari mpya, maarifa ya kurejea Simba ninayoitaka, naongozwa zaidi na ushabiki, wala siyo ufadhili na uwekezaji, sitoiacha Simba leo wala kesho," alisisitiza.

Mo alitangaza kujiuluzu nafasi yake Septemba, mwaka 2021 na kumteua Tyr Again, ambaye kipindi hicho alikuwa ni makamu wake kuongoza jahazi hilo la Wekundu wa Msimbazi.

„Kuna baadhi ya wachezaji siyo waaminifu, hawajitumi na kuitendea haki klabu yetu, viongozi wanaokuja wanapaswa kuwachukulia hatua kali ambazo zitafanya kila mchezaji kuwajibika. Tunasajili wachezaji kwa pesa nyingi, tunalipa mishahara lakini si waaminifu, niseme tu, nitaongea na uongozi mpya ili kuwachukulia hatua hawa ambao si waaminifu," alisema Try Again wakati anatangaza kujiuzulu.

## Yanga yajiuliza, Azam yajitoa Kagame Cup

INATOKA UK. 24

kuanza Agosti, Azam FC itakuwa tayari kushiriki michuano hiyo.

Timu nyingine kutoka Bara zitakazoshiriki michuano hiyo ni Simba na Coastal Union wakati TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Red Arrows (Zambia) na Nyasa Big Bullets ya Malawi ni timu waalikwa.

APR ya Rwanda, El Merreikh, Hai El Wahdi, El Hilal (Sudan), Gor Mahia (Kenya), SC Villa (Uganda), El Merreikh Bentiu (Sudan Kusini) na JKU ya Zanzibar, pia zimetajwa kushiriki michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Express ya Uganda ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo baada ya kuwafunga Nyasa Big Bullets bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam mwaka, 2021.

Michezo
Nipashe
Alhamisi Juni 13, 2024

## Southgate: Nitaondoka nisiposhinda Euro 2024



UKURASA 21



Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakishangilia baada ya kuwafunga wenyeji Zambia katika mechi ya Kundi E ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa ulioko Ndola juzi usiku. Stars ilishinda bao 1-0. **PICHA: TFF**

# SINEMA YAKOLEA SIMBA

## Mo Dewji, Try Again warejea, mwekezaji aja na mikakati sita maalumu...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Mwekezaji na Rais wa Heshima wa Simba, Mohamed Dewji ‚Mo Dewji' amerejea katika nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi na kusema amekuja na mikakati sita itayoiwezesha timu yao kuimarika, Salim Abdallah ‚Try Again' naye amerudi ndani ya uongozi wa klabu hiyo, muda mchache baada ya kutangaza kujiuzulu.

Akizungumza muda mchache baada ya Try Again kujiuzulu, Mo Dewji, alisema amerejea na nguvu mpya na atahakikisha kikosi cha Simba kinarejea katika ubora wake kama ilivyokuwa miaka mitatu iliyopita.

Mo alisema kufanya vibaya kwa Simba katika misimu miwili iliyopita kumetokana na usajili mbovu wa wachezaji pamoja na kuwa na benchi la ufundi lisilokuwa na viwango.

Mfanyabiashara huyo amewahakikishia wanachama na mashabiki wa Simba ataendelea kuwa mwekezaji na hatatoka leo wala kesho kama baadhi ya watu wanavyodhani kwa sababu uwepo wake ndani ya klabu hiyo ‚unabebwa' zaidi na ushabiki, wala si uwekezaji au ufadhili.

Alisema kilichoifelisha Simba msimu huu ni kushindwa kutengeneza timu ya ushindani na hiyo ilitokana na kusajili idadi kubwa ya wachezaji wenye viwango vya chini ambavyo hakikufanana na hadhi ya klabu hiyo.

„Kwanza kabisa hatukuwa na umoja, hasa baada ya uchaguzi, malumbano na mgawanyiko umeendelea kututafuna, jambo hili halina afya, niwaombe tumalize tofauti zetu za uchaguzi na kuzikika kabisa.

Pili, tumeshindwa kutengeneza timu bora ya ushindani, eneo la benchi la ufundi halikuwa zuri, imesababisha hata kupoteza falsafa yetu ya pira-biriani, hili ni eneo muhimu la kufanyia kazi, naahidi tutashirikiana na wenzangu kusuka upya eneo hilo na tatu.

Tumeshindwa kukidhi kiu ya Wana-Simba katika usajili, nyota wengi waliosajiliwa viwango vyao havikuwa bora, kwa hiyo ningependa kuwaahidi, nitashirikiana na viongozi wenzangu, pamoja na wataalamu kufanya usajili bora, katika ukubwa utakaokidhi matamanio ya wanachama na mashabiki," alisema Mo.

Aliutaja mkakati wake wa nne ni kushirikiana kwa karibu na wanachama, mashabiki na viongozi wenzake kukamilisha mchakato wa mabadiliko ya uendeshaji ndani ya klabu hiyo, ili watu waanze kupata hisa za umiliki.

„Lingine ni eneo la ukuaji wa wanacha-

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yajiuliza, Azam FC yajitoa Kagame Cup 2024

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga umesema utatoa taarifa rasmi kuhusiana na ushiriki wao katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kagame Cup yaliyopangwa kufanyika kuanzia Julai 6 hadi 22, mwaka huu hapa nchini.

Mpaka jana Yanga ilikuwa haijathibitisha sambamba na Azam FC, kushiriki michuano hiyo itakayofanyika kwenye viwanja vya Tanzania Bara na Zanzibar.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema uongozi wa klabu hiyo utaweka hadharani uamuzi waliofikia kuhusu mashindano hayo hivi karibuni ili kila mwanachama afahamu mustakabali wao.

„Uongozi unajiandaa kutoa tamko la klabu, wanachama na mashabiki watulie, tutatoa tamko letu rasmi kuhusiana na mashindano haya," alisema kwa kifupi Kamwe.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia ‚Zaka Zakazi' aliliambia gazeti hili timu yao haitashiriki mashindano hayo kwa sababu ya muda uliopangwa kutokuwa rafiki.

Zaka alisema wachezaji wao wameenda mapumziko na watarejea rasmi kuanza maandalizi ya msimu mpya Julai 4, mwaka huu.

„Ili timu iweze kukuonyesha kitu inahitaji kufanya mazoezi ya pre season kwa muda wa wiki sita, sasa sisi tutaanza kambi siku mbili kabla ya kuanza mashindano, na hapo wachezaji wanarejea wengine wakiwa na vitambi," Zaka alisema.

Hata hivyo aliongeza endapo ratiba ya mashindano hayo itabadilika na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042